

MFALME ALIYEKATALIWA

 Nilikuwa mapema kidogo tu usiku wa leo. Nami nikasikia ya kwamba Ndugu Sullivan na... walikuwa wamechukua sa—sadaka ya upendo kwa ajili yangu. Sasa, hakika ninathamini hilo kwa moyo wangu wote, enyi marafiki. Kama hamngekuwa mmefanya hivyo, ingekuwa sawa tu, haijalishi.

² Nimeninii... Nimekuwa hudumani kwa karibu miaka thelathini na mmoja, wala sijawahi kuchukua sadaka kwa ajili yangu binafsi, bado, wala kwa ajili ya mtu mwingine yeyote, kamwe sikuchukua moja; na watu wananipa sadaka. Na jinsi sadaka hiyo inavyotumika, inaingia moja kwa moja kwenye wakfu wa maskani. Na kutoka hapo inatumika kwa safari za ng'ambo, na kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Mimi nina mshahara, ninapata dola mia moja kwa juma, hizo ndizo ninazopata. Wala sina ninii yoyote...

³ (Nilifikiri mtu fulani huko nje, ndugu, angeninii, huenda... Nilikuwa nikijaribu kuishikilia ili kinasauzi, niliwazia, labda...) Hizo ni bendeji nyingi kuliko daktari alizo nazo ofisini wake, siyo? Asante, ndugu. Kwa sababu haitampungukia mtu yeyote *huko* nje, iko *hapa*.

⁴ Kwa hiyo basi, kadiri niwezavyo, kwa yote niujuayo, nitahakikisha ya kwamba kila senti yake inaenda kwa Ufalme wa Mungu, kwa yote niujuayo, maana ni sehemu ya riziki yenu. ninajua hakuna mamilionea miongoni mwenye, nanyi mnahitaji kila peni mnayoweza kupata.

⁵ Kitu hicho kina kichwa dhaifu, siyo? Nami nawaambia, nitaegemeza tu Biblia yangu kwake. Vipi hivyo? Vema. Hilo litatosha kwa muda kidogo, labda. Nitakurekebisha, ndugu. Tuna kitu fulani hapa. Haya basi. Vipi hivyo? Gango dogo, wakati mwingine sote tunahitaji hilo, kwa namna fulani kujikaza, mwajua, “kujizatiti,” tunavyosema, mwajua.

⁶ Na kwa hiyo, ninalithamini, na nitafanya kila niwezalo kuhakikisha kwamba inatumika kwa ajili ya Ufalme wa Mungu.

⁷ Sasa, loo, jamani, hii hapa bendeji nyingine. Sasa, Ndugu Sullivan, kweli tutamfunga jamaa huyu vilivyo, siyo? Jamaa muhimu! [Ndugu Sullivan anasema, “Hapana shaka yeye ni mmoja wa hao wavulana.”—Mh.] Hapana shaka yeye ni mmoja wao, bila shaka yeye ni mmoja wao. Loo, nilikuwa nikimkatiza mtu, hakika kabisa. Nilikiweka hicho Kitabu juu ya maikrofoni moja ama mbili hapa. Tunanyang'anya moja kuilipa nyingine. Asante sana, ndugu. Nina hakika yeyote yule anayekimbilia kule chini atathamini hilo.

⁸ Leo imekuwa ni siku kuu kwangu, tumekuwa na mengi. Nami nina matangazo machache hapa ninayotaka kutoa. Jambo

la kwanza ni kwamba, ninyi nyote mmealikwa asubuhi kwenye Kiamshakinywa cha Ushirika wa Wafanyabiashara Wakristo. Sikuzote tunakuwa na wakati mzuri sana kwenye mkutano huo. Huo utafanyika kwenye Hoteli ya Manchester, nafikiri kwenye bwalo, ama... Na tiketi zinauzwa, unaweza kumwona Ndugu Carlson, ama katibu wangu wa huduma, Ndugu Mercier, ama Ndugu Goad papa hapa, wanazo hizo tiketi za kiamshakinywa.

⁹ Na usipowaona, shuka uje, kutakuwako na mtu pale kukupa tiketi asubuhi. [Ndugu Sullivan anasema, “Ndugu Rockwell anazo...—Mh.] Wasemaje? [“Ndugu Rockwell anazo, pia.”] Ndugu Rockwell anazo, pia. (Kuna mtu mwingine unayemjua? Hivyo—ndivyo hivyo.) Lakini ukiikosa, kutakuwa na mtu huko asubuhi kwenye, ukumbini kukuwezesha kupata tiketi. Na Bwana akipenda, nitakuwa nikizungumza asubuhi kwa ajili ya ushirika huu.

¹⁰ Ninapenda Ushirika wa Wafanyabiashara Wakristo kwa sababu unatetea kile ninachoamini: ushirika wa baina ya madhehebu. Nao wanaidhamini mikutano yangu sana kote ulimwenguni, kwa sababu katika hiyo ninayaacha ninii, makanisa yote ku—kudhamini, kwa sababu ushirika wa—wao, watu wa—wao, ninii yao, huko ni nje ya makanisa yao, wafanyabiashara walio makanisani mwao wanaingia katika shirika hili. Ndipo wakati mwingine inawabidi kunipokea wanipende wasinipende, inawabidi tu kunipokea, kwa vyovyote vile, maana ndugu za—zao wako mle ndani.

¹¹ Lakini karibu sikuzote, namshukuru Bwana, kwamba hata katika wahudumu na katika makanisa wanaoona tofauti, baadhi ya watu ambao hata hawaamini katika tukio la Kipentekoste wataingia moja kwa moja na kusaidia kudhamini mkutano, kwa vyovyote vile. Nimekuwa na... Nimedhaminiwa na Wabaptisti, Wamethodisti, Walutheri, Wapresbiteri, wa namna zote mbalimbali. Huko chini Meksiko, nafikiri udhamini wote ulikuwa wa Baptisti, huko chini katika Jiji la Meksiko.

¹² Halafu sehemu nyingi za—sehemu nyingi ni za Kilutheri. Huko Uswidi sasa hivi, nafikiri ndivyo ilivyo, ama Norwe, makanisa ya Kilutheri yanataka kudhamini uamsho kamili—kamili wa nchi nzima. Huko chini Puerto Rico moja ya kundi la Billy Graham lililomdhamini, yule aliyekuwa mkalimani wake alikuja mkutanoni, naye Bwana akafanya jambo kubwa; hapo tu siku mbili usiku. Na sasa shirika lote la wahudumu kote kisiwani, wako tayari kwa mkutano wa kisiwa chote.

¹³ Nilipokuwa nikiondoka asubuhi hiyo, kulikuwako na yule jamaa aliyekuwa mkuu wa ule uwanja mkubwa wa ndege huko nje akakimbia na kunikumbatia kwa mikono yake, akaanza kulia, maskini mtu mdogo wa kimo, akasema, “Ndugu Branham, ulipokuwa hapa yapata mwaka mmoja uliopita kwa siku moja au mbili usiku,” kasema, “Nilikuwa nimeketi huko nyuma kabisa

kwenye kusanyiko. Nawe ukataja jina langu, na kuniambia nimekuwa na maumivu ya kichwa ya kipandauso kwa miaka mingi. Na kusema, 'BWANA ASEMA HIVI, usiku wa leo yamekwisha.'" Kasema, "Sijawahi kuwa na moja tangu wakati huo." Mnaona? Kisha kasema. . . Naye alikuwa ndiye mkuu wa uwanja huo wa ndege, afisa mashuhuri huko nje, nisingesema kiongozi wake, alikuwa mmoja wa watu wakuu huko nje.

¹⁴ Katika mahojiano asubuhi ya leo, Bwana alitoa maono mengi; nami nilikuwa, bila shaka nilikuwa na kundi asubuhi ya leo. Tunatumia asubuhi katika mahojiano kushughulikia visa ambavyo haviwezi. . . visa vya dharura tu na mambo kama hayo, ambapo hawana budi kupata kitu kutoka kwa Bwana, Neno la Bwana. Na kwa hiyo basi, Bwana amekuwa mwema sana kwetu katika mambo hayo.

¹⁵ Basi mtu mmoja alikuwa akiniambia, sikumbuki kisa hicho, wala nisingekijua isipokuwa nikipate tena kwenye kanda, mtu fulani kutoka huko chini Kusini, ninaamini Alabama, mahali fulani, usahihi wa Roho Mtakatifu akimwambia mama huyo kwamba alikuwa ni nani, jina lake lilikuwa nani, yale aliyokuwa amefanya, jinsi alivyokuwa ameumia akiwa msichana mdogo, akamwambia mji aliotoka na yote kulihusu, na wakati ilipoanza kulitaja jina lake, ilimwita Binti, naye alikuwa ni mwanamke wa makamu, ila hajapata kuolewa, ni usahihi tu wa Roho Mtakatifu, jinsi afanyavyo hayo.

¹⁶ Halafu asubuhi ya leo katika mahojiano, pale, nadhani wako hapa, ni wamishenari kadhaa waliokuwa mahali fulani mkutanoni, sikutaja jina lao hapa chini, bali walikuwa kwenye mahojiano asubuhi ya leo, na kusema yapata wakati fulani uliopita walikuwa katika mmoja wa mikutano, naye huyo mama alikuwa anateseka sana na kitu fulani, na—naye mumewe, pia. Naye akasema ilimwambia yeye alikuwa ni nani na alikuwa anaumwa na nini; akamwambia mumewe shida yake na mambo yote walivyokuwa wamefanya maishani, na ulipokuwa wito wao, nao walikuwa wakienda kuwahudumia watu waliovaa kofia ndogo kichwani mwao, ambao walikuwa ni Wayahudi, nao walikuwa wakienda ng'ambo, na kila kitu kingetukia. Naye akasema, "Kila kitu jinsi kilivyokuwa hasa, kilikuwa sahihi."

¹⁷ Ndipo akasema basi aliporudi alikuwa ameshikwa na ugonjwa, naye akasema ya kwamba yeye. . . madaktari walitaka kumfanyia upasuaji kwa ajili ya namna fulani ya shambulizi kwenye nyongo, ama kitu fulani. Nao walitaka kumfanyia upasuaji mara moja, lakini akarudi upande huu, kama nikipata hadithi hii vizuri, basi kusema, akaomba, "Ee Bwana, ninaenda kule." Alikuwa amepata moja ya magazeti mahali ulipopaswa kuwa. Ndipo akasema, "Bwana, mara ya mwisho nilipokuwa kule nilipata kadi namba tatu. Tafadhali, Bwana, nijalie nipate kadi namba tatu tena."

¹⁸ Kisha akasema—kisha akasema Roho Mtakatifu alionekana kumwambia...Yeye ni Mkristo, nafikiri zamani alikuwa Mlutheri, na nesi kutoka hospitalini. Ndipo kasema Bwana alimwambia, “Utapata kadi namba tatu.” Akasema usiku huo wakati mwanangu alipokuja kugawa kadi, kwa hiyo itakuwa maradufu tutakapoitisha mikutano kwamba hakuna mtu atakayejua, Billy hana budi kusimama mbele ya umati na kuchukua hizo kadi na kuzichanganya zote pamoja, ili watu wajue.

¹⁹ Halafu jambo lingine, hakuna mtu anayejua mahali tutakapoanzia mstari wa maombi, mimi huja, na popote Roho Mtakatifu anaponiongoza, ninaanzia hapo.

²⁰ Kwa hiyo, wakasema alisimama, akazichanganya hizo kadi zote kisha akashuka chini. Akasema, “Nataka moja.” Akamkabidhi, naye akapita tu. Akaiangalia, ilikuwa—ilikuwa ni tisini na nane, naamini, ama, tisini na saba, naamini, naam, tisini na saba nafikiri ndiyo.

²¹ Naye akasema, “Loo, Bwana, uliniahidi namba tatu, na sasa Wewe unanipa tisini na saba,” ama chochote kile, tisini na saba, tisini na nane, tisini na saba nafikiri ndiyo ilikuwa. Kasema, “Umenipa tisini na saba,” kisha kasema, “sasa, uliniahidi namba tatu.” Basi akasema alianza kulia, wala hakujua la kufanya, kasema, “Kamwe sitaitwa kwenye tisini na saba.”

²² Kwenye ule wakati aliokuwamo huenda nilianza kutoka kwa moja. Kasema usiku huo nikija jukwaani, kasema, niliangalia huo umati kwa ukali sana, na kusema, “Nitaanzia usiku wa leo kutoka mia moja na kurudi nyuma.” Namba tatu!

²³ Huyu mama yumo humu jengoni? Kitu gani?...?...Loo, huyu papa hapa mbele yangu. Loo, Bwana akubariki, dada. Roho Mtakatifu daima yuko sahihi, sivyo? Hiyo ni kweli. Bwana awabariki.

²⁴ Vema hilo ni sawa. Mnaona, Roho Mtakatifu anapokuahidi chochote, kama ni Roho Mtakatifu, utakipata, kama tu Yeye alivyosema. Haidhuru ni jambo gani linalotukia, utakipata.

²⁵ Sasa, kwenye mkutano huu, Ndugu Sullivan, Ndugu Boze, Ndugu Winston, na wahudumu wote, na watu wote, ninataka kuwashukuru kwa ushirikiano wenu mzuri wa...Kwangu mimi, mmoja wa mikutano mizuri sana niliyowahi kuhubiria maishani mwangu mwote umekuwa ni huu. Nimekuwa na uhuru zaidi wa kuzungumza kwa uhuru bila kufungwa hata kidogo, nilijisikia nyumbani kabisa, kana kwamba nilikuwa nimesimama maskanini mimbarani, katika kanisa langu mwenyewe. Nami nilijisikia vizuri zaidi kuliko, katika mkutano huu, kuliko nilivyojisia katika wowote, nami...kadiri niwezavyo kukumbuka. Umekuwa ni mmoja ambao kamwe sitausahau. Bwana awabariki kwa maombi na ushirikiano wenu. Na hakika ninalithamini.

26 Ni ninii yangu...nikitazamia kuwa pamoja nanyi tena mwaka ujao, Bwana akitujalia, tena popote utakapofanyiwa, sijui, Bwana atajalia hilo. Nami nataka kusema ya kwamba, hakika ninathamini hili na ninathamini mkutano huu, kwa sababu...

27 Sasa, nimeshutumiwa kuwa ninapinga makanisa ya kidhehebu, lakini hilo ni kosa, sipingi chochote ila dhambi. Mnaona? Ni—ni—ninaninii tu...Mimi sipingi dhehebu lolote, wala watu wowote, mimi ni Mmethodisti tu kadiri nilivyo Mbaptisti, Mpentekoste, chochote kile, mimi ni ndugu yenu. Ni—ni—ni—ninaninii tu...Haileti tofauti yoyote.

28 Sasa, wakati mwingine ninayakemea madhehebu sana, ni kwa sababu ya msimamo wao wa kichoyo, wanapojivuta wakaingia katika ganda dogo, na kusema, "*Tunalo*, hakuna mmoja wenu anayeweza *kulipata*."

29 Huwezi kuiundia Pentekoste dhehebu. Na tunapojaribu kuunda dhehebu kutoka kwa Pentekoste, tunamchukiza Mungu. Tunajiita dhehebu *hili* la Kipentekoste, *lile* la Kipentekoste, lakini hilo ni kosa. Pentekoste ni tukio, wala si dhehebu. Na kwa hiyo, lakini wakati mwingine makundi mbalimbali huyapanua makundi yao, na ni tamshi la kilimwengu tu. Lakini katika kila kundi ambalo nimewahi kuingia maishani mwangu, nimekuta wanaume na wanawake wa kweli waliojazwa na Roho Mtakatifu. Naam, bwana, kwa hayo yote.

30 Na mkutano huu daima na ushikilie kiwango chake cha kujitegemea. Ili kwamba ninyi...makundi yote yaweze kukusanyika pamoja, Wapentekoste huru, na Wabaptisti huru, Wamethodisti huru, na loo, Umoja, Uwili, Utatu, na hao wengine wote, na—na wamepanda ngamia mwenye nundu moja, ngamia mwenye nundu mbili, ama ngamia mwenye nundu tatu, chochote unachotaka kupanda, njoo.

31 Mwajua, Yakobo alichimba kisima kimoja nao Wafilisti wakamfukuza kutoka kwake, naye akakiita, naamini, "Kijicho," tutasema hivyo, sikumbuki tu lilikuwa gani. Akachimba kisima kingine, nao Wafilisti wakamfukuza kwake, uh, wakamfukuza, naye akakiita, "Ugomvi." Ndipo Yakobo akachimba kisima kingine, naye akakiita, "Ipo nafasi kwa wote."

32 Hicho ndicho kile kisima, hicho ni kile cha walio huru, ambapo pana nafasi kwa wote, kila mtu, yeyote atakaye, kanisa lolote, kanuni yoyote ya imani, dhehebu lolote. Tuko hapa kuwakilisha baraka za Kipentekoste zinazowajia Wamethodisti, Wabaptisti, Katoliki, Myahudi, chochote ulicho. Inawajia wa manjano, weusi, weupe, wa kahawia, jamii zote, kanuni zote za imani, watu wote wakati wowote ambao mko tayari kwa ajili yake. Daima na ibaki hivyo, ndilo ombi langu.

33 Sasa, msisahau, usiku wa leo unamalizia huu mkutano. Nao ndugu watakuwa wakienda nyumbani, wengi wao, nadhani.

Sasa, sikujua ya kwamba nilikuwa ninaenda kuwaombea wagonjwa u—usiku. Kwa hiyo niliwazia ningekaa zaidi ya siku mbili usiku ili kuwaombea wagonjwa wanaokuja mkutanoni. Lakini niliona kwenye matangazo madogo kule chini, niliyoona yametundikwa kwenye dirisha la kituo cha petroli, yaliyosema, “Maombi ya wagonjwa kila usiku.” Niliyaona hayo wakati mimi na Ndugu Joseph jana tulipokuwa tukipita. Kwa hiyo basi jana usiku tukaanza kuwaombea wagonjwa; sikujua ya kwamba nilipaswa kuwaombea wagonjwa. Kwa hiyo basi, kama uko hapa, nawe huna haraka kufika nyumbani, bila shaka umekaribishwa kukaa pamoja nasi Jumamosi usiku na Jumapili alasiri.

³⁴ Tutafunga Jumapili alasiri, kwa sababu hatutaki kuwazuia watu kutoka makanisani mwao Jumapili usiku. Kwa dhehebu lako na kwa kanisa lako utakalochagua, hilo ni jukumu lako kusimama kwenye wajibu wako, hasa, kwa mchungaji wako, na kumshikilia kama mtu wa Mungu. Kama yeye bado haoni Nuru, usije ukaachana naye, mpende na kumwombea, hilo ndilo jambo la kufanya upate kumwingiza ndani yake. Hiyo ni kweli.

³⁵ Kama wewe ni . . . Kama wewe una kanisa lisiloamini katika baraka za Kipentekoste, vema, hilo halidhuru kitu. Wewe endelea moja kwa moja na uendele . . . Ukipokea baraka za Kipentekoste, basi mwambie mchungaji wako juu yake na umwambie jinsi zilivyo tamu, na muda si muda wajua atakuwa kama Ndugu Collins hivi majuzi usiku, yule mhubiri wa Kimethodisti, alipompokea Roho Mtakatifu. Ilimbidi kwenda kumchukua ndugu yake, na shemeji yake, na hao wote, wakampata Roho Mtakatifu. Kwa hiyo, hivyo ndivyo tu linavyoenda. Unaona?

³⁶ Kamwe hatutaki kumchukua mtu yeyote kutoka kwa kanisa lolote. Hatutaki kusema, “Hebu hilo kanisa lote *moja* lijiunge na kanisa hili *lingine*.” Hilo silo. Kaa papo hapo ulipo. Hilo ni sawa. Mradi tu watakupokea nawe una baraka, wewe kaa papo hapo ulipo. Lakini jaribuni kufanya ushirika ninyi kwa ninyi. Hivyo ndivyo ilivyo, ni ushirikiano wa ndugu, ndugu kushirikiana. Ninaamini kila mtu anaamini hilo, sivyo? Hakika. Hilo ni sawa.

³⁷ Sasa, nilikuwa nikitaka kutangaza kile nitakachozungumzia kesho asubuhi, lakini a—afadhali niachane nalo, maana mimi—mimi—mimi husema nitazungumza juu ya jambo fulani, kisha nikifika huko napata kitu kingine. Mnaona? Nina ninii tu . . . Mimi, kama ningeweza kuhubiri kama nifanyavyo ninapokata nyasi zangu, ama nikienda kuwinda mahali fulani, hupanda milimani, na kupanda juu ya milima, na kusimama huko juu na kuangalia upande wa pili na kuhisi upepo huo huko juu milimani, na kusikia mbwa mwitu akilia, whiu, jamani! Kama ningeweza kuhubiri kama vile ningeweza papo hapo, niketi chini juu ya mwamba huo, kisha nitoke kwenye huo mwamba, na kuuzunguka huo mti na kuhubiri, na kupiga makelele,

kama ningeweza kuhubiri namna hiyo hapa juu, ningekuwa—ningekuwa mhubiri mzuri sana, naamini.

³⁸ Ninapoenda uani nikikata nyasi, basi inanibidi tu kuzima wakati mwingine, ninazima mashine yangu ya kukata nyasi na kukimbia kwenye gereji, na kusema, “Bwana, nisaide. Sitaki kutenda namna hiyo huko nje uani, watu watafikiri nimerukwa na akili.” Lakini basi ninapofika hapa, ninasahau yote kuyahusu, “Nilikuwa nikiwazia nini?” mnaona, basi inanibidi tu kumtegemea Yeye. Kwa hiyo hiyo ndiyo sababu wakati mwingine siwezi kusema yale nitakayozungumzia, bali Bwana atanisaidia kufanya jambo fulani, hata hivyo.

³⁹ Sasa, hebu na tufungue usiku wa leo kwenye, kwa ajili ya somo, kama ningeliita hivyo, katika Samweli wa Kwanza mlango wa 7, ama, mlango wa 8, na kuanzia kifungu cha 4. Samweli wa Kwanza mlango wa 8, na ninii, kuanzia kifungu cha 4. Hebu tusome:

Ndipo wazee wote wa Israeli wakakutana pamoja, wakamwendea Samweli huko Rama,

Wakamwambia, Angalia, wewe umekuwa mzee, na wanao hawaendi katika njia zako: basi tufanyie mfalme atuamue, mfano wa mataifa yote.

Lakini neno hili likawa mbaya machoni pa Samweli, waliposema, Tupe mfalme atuamue. Naye Samweli akamwomba BWANA.

BWANA akamwambia Samweli, Isikilize sauti ya watu hawa katika kila neno watakalokuambia: kwa maana hawakukukataa wewe, bali wamenikataa mimi, ili nisiwe mfalme juu yao.

Kwa kadiri ya matendo yote waliyotenda tangu siku ile nilipowapandisha kutoka Misri hata leo, kwa kuniacha mimi, na kwa kuitumikia miungu mingine, ndivyo wanavyokutendea wewe.

⁴⁰ Kama ningetaja kichwa cha hili, kwa dakika chache... halafu tutachukua kadi zetu kwa ajili ya kuwaomba wagonjwa pale pale tulipoachia jana usiku. Halafu kesho usiku... kesho alasiri kadi za maombi zitasambazwa, mstari mwingine wa maombi kesho usiku. Halafu Jumapili saa nane? [Ndugu mmoja anasema, “Saa nane na nusu.”—Mh.] Saa nane na nusu, kadi za maombi zitasambazwa saa nane basi, Jumapili alasiri kwa ajili ya ibada ya Jumapili alasiri, tukiwaomba wagonjwa.

⁴¹ Ninataka kuliita somo hili usiku wa leo: *Mfalme Aliyekataliwa.*

⁴² Na laiti tungalikuwa na viti kuwaketisha watu au vya kukalia, kwa namna fulani, wale wanaosimama kote usiku huu kwenye jengo hili, lakini nitajaribu kuharakisha kusudi

isiwabidi kusimama kwa muda mrefu sana. Lakini laiti mngalinipa tu usikivu wenu wote kwa dakika chache.

43 Katika siku za Samweli watu walikuwa zaidi sana kama walivyo siku zote, walikuwa wamefikia mahali ambapo walitaka kuwa kama watu wengine. Na hiyo kwa urahisi tu ndiyo tabia ya watu, watu wanataka kuiga tabia za wao kwa wao.

44 Kama utatoka uende kununua nguo ya aina fulani, ama motokaa fulani, upake vipandio vyako rangi fulani nyumbani mwako, ama kwenye vipandio vyako, vipandio vya ukumbi, mwangalie jirani, kamwe hawawezi kuvumilia hilo, hawana budi kuwa vivyo hivyo.

45 Unaenda kanisani na kuvaa aina fulani ya kofia ambayo ni tofauti kidogo, Jumapili ijayo utakuwa na dada zako wengi walio na kofia aina hiyo, kama wanaweza kuipata. *Kwa namna fulani* wanataka tu kutenda kama wengine. Na hilo ni jambo zuri kama likitumiwa vizuri, kama likitumiwa kwa njia ifaayo.

46 Sasa, lakini watu hawa katika siku za nabii Samweli, walitaka kutenda kama Wafilisti, na Waamaleki, na wasioamini, nao, kwa sababu waliona watu wao walikuwa ni wa kuvutia zaidi. Nao walikuwa taifa la watu walioitwa watoke na waliochaguliwa, nao hawapaswi kutenda kama watu wengine.

47 Watu wa Mungu hawapaswi kamwe kutenda kama walimwengu, ama kuonekana kama walimwengu, au kuwa na uhusiano wowote na walimwengu. Ninyi ni watu waliotengwa, Kanisa, walioitwa watoke, watu wa kipekee, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, kwa jumla ni tofauti kabisa na kutengwa katika matendo yenu yote, na tabia, na njia kutoka kwa mambo ya ulimwengu. Sasa, Bwana na atusaidie tunapojifunza.

48 Sasa, watu hawa waliona jinsi Wafilisti walivyokuwa wakifanya, jinsi Waamaleki, na wengine mbalimbali walivyokuwa wakitenda, nao wakamjia Samweli, na kusema, “Tunataka kuwa kama wao.”

49 Na ni karibu vivyo hivyo leo. Hebu acha tu ulimwengu uanzishe mtindo fulani, ama—ama kivutio fulani, na utaona watu wote, hata kwa wengi wa Wakristo wanataka kufanya jambo lilo hilo, wanataka kutenda hivyo.

50 Hebu wavulana waanze kukata nywele zao kwa njia fulani, na wavulana wote wanataka kufanya hivyo. Nao wamefikia mahali fulani sasa, wanaacha nywele zao zikue kubwa sana, na kuonekana kama bata, ama chochote kile, ameketi juu ya kichwa chao. Nami nawaambia, ninaamini ya kwamba mimi—mimi . . . kama—kama ningalikuwa mwanamke, msichana, na mvulana mpenzi wangu afanye hivyo, ningemkeitisha chini na kunyoa nywele zake. Inaonekana kwangu kana kwamba mwanamke angetaka mwanamume.

⁵¹ Nawaambia, labda mwanamke huyo ni wa kiume sana, hata anataka kitu cha kike, lakini hakika huyo anaonekana kama mwanamke kwangu mimi. Wana kichaka hicho kikubwa, kama bata, ama kunguru, ama chochote kile, kimeketi juu ya kichwa chao, hicho kitu kikubwa, kirefu kinachotokeza huko nyuma, wala sijawahi kuona vazi kama hilo maishani mwangu. Nami niliona baadhi ya wahubiri kama hao. Kitu hiki kinaelekea wapi? Baada ya kitambo kidogo watakuwa na mchungaji wa kihuni, kama hutaangalia wanachofanya. Vema, huo ndio ukweli.

⁵² Loo, kanisa halina budi kutenda tu kama ulimwengu. Halina budi kuwa . . . Sasa, hilo lilikuwa ni fidhuli, nami si—simaanishi hivyo, mnaona, lakini ninajaribu tu kufanya ninii . . . Ninajaribu kuupigilia msumari sana hata hautang’oka, mpaka ushikilie upande wa pili. Kama unaumiza, labda utachomoka tu kidogo. Lakini hauna budi kupigiliwa upate kushikilia. Hiyo ni kweli, Ndugu Wood? Yeye ni mkandarasi. Inakubidi kuufanya ushikilie kwa kuupigilia.

⁵³ Nami na—nafikiri mwanamume anapaswa kuwa mwanamume, na mwanamke anapaswa kuwa mama wa heshima. Nami nafikiri ya kwamba Mkristo anapaswa kutenda kama Mkristo, na kushirikiana na Wakristo. Nalo Kanisa la Mungu aliye hai linapaswa kuwa pamoja kwa moyo mmoja, na nia moja, wala lisiwe na uhusiano wowote na ulimwengu, inapofikia njia na tabia zao. Lakini tunaliona siku hizi kama tu lilivyokuwa wakati huo.

⁵⁴ Walimjia Samweli, nao wakasema, “Sasa, unazeeka, nywele zako zinaingia mvi, na sisi—sisi kamwe hatujui utakaa huku muda gani zaidi. Na sasa, tunataka utufanyie mfalme kama tu Wafilisti walivyo naye, na kama walimwengu wengine wote walivyo nao. Tufanyie tu kama wao.”

⁵⁵ Nalo likamchukiza huyu nabii mtakatifu wa Mungu. Nabii yeyote, kama yeye ni nabii, atashindania utakatifu, na haki, na mambo ya Mungu, hawezi kusimama kimya, hana budi kuyakemea. Wakati mwingine inagharimu maisha yake, bali ye—ye—yeye atayakemea, kwa vyovyote vile, kwa sababu Mungu yuko ndani ya mtu huyo. Naye mchungaji ama nabii ambaye kweli ni wa Mungu, kama linaudhi, inaninii tu . . . Ha—hakusudii kuwaudhi watu, anawapenda watu, bali anajaribu kuwaokoa. Mnaona?

⁵⁶ Na mbona, hili kwa namna fulani lilimwudhi maskini nabii huyo mzuri, kwamba walidhani alikuwa ni mzee sana asingeweza kuendelea. Tunaona ya kwamba aliishi miaka mingi, mingi sana baadaye. Lakini alikuwa—alikuwa mtumishi wa Bwana. Na katika kufanya hivyo, walimkataa Mfalme wao halisi ambaye alikuwa ni Mungu, na hilo lilimchukiza huyo nabii, wala hakutaka wafanye hivyo.

⁵⁷ Sasa, Samweli, katika ujumbe wetu, anamwakilisha Roho Mtakatifu. Sasa, Samweli alikuwa ndiye msemaji wa Mungu. Na, leo hii, Roho Mtakatifu ndiye kinywa cha Mungu. Na, leo hii, badala ya kuwa na madoido yetu yote mbalimbali kanisani, Mungu anatutaka tumwache Yeye atawale, sio mapapa, maaskofu, na waangalizi wakuu, na mafundisho, na madhehebu, na kila kitu, alimtuma Roho Mtakatifu kulitawala Kanisa.

⁵⁸ Lakini sisi, kama watu wa kale, tunasema, “Vema, hebu na tuwe kama hao wengine. Wana dhehebu kubwa, hebu na tulijenge kundi letu, kwa sababu tunaamini *hili*.”

⁵⁹ Sasa, Roho Mtakatifu kamwe asingalivumilia hilo. La, bwana. Roho Mtakatifu anatutaka tusiwe na nyua, tusiwe na mipaka, Yeye anatutaka tuwe mmoja ndani Yake. Sisi ni watoto, ndugu. Mungu hawatenganishi watoto Wake, aseme, “Nitampa *huyu* mkate mmoja wa mahindi na maharagwe, na *huyu* aiskrimu moja na sambusa.” Yeye hafanyi hivyo. Aache *huyu* afe kwa njaa, na kitu hicho kingine, Yeye huwalisha wote kwenye meza moja. Naye Roho Mtakatifu anapaswa kuliongoza kanisa.

⁶⁰ Lakini hawakutaka iwe hivyo, wa—walitaka mfalme, walitaka kuwa kama walimwengu wengine. Na wakati kanisa la Kipentekoste, Roho Mtakatifu aliposhuka kwa mara ya kwanza yapata miaka hamsini na kitu iliyopita, kama wangeliachilia tu na kumwacha Mungu aongeze Kanisani kila siku wale waliokuwa wakiokolewa, ingekuwa kama ilivyokuwa katika wakati wa kimitume. Lakini ilitubidi kujenga nyua, ilitubidi kujifananisha na hao wengine, ilitubidi, “Kama Methodisti ni dhehebu, hatuna budi kuwa.”

Kisha huyu hapa mtu mmoja anakuja, akisema, “Yesu yuaja juu ya wingu jeupe.”

“La, Yeye anakuja amepanda farasi mweupe.”

“Vema, tutatengana tu. Nitajichukulia kundi, nawe ujichukulie kundi.”

⁶¹ Haya basi. Inaleta tofauti gani? Anakuja, kwa vyovyote vile. Wala haijalishi jinsi anavyokuja, jambo ni kwamba, je, uko tayari kwenda pamoja Naye atakapokuja? Hilo ndilo jambo muhimu. Haijalishi jinsi anavyokuja, kwamba anakuja katika umbo gani, hebu tuwe tu tayari kwenda. Lakini watabishania tofauti ndogondogo na kuunda dhehebu lingine. Na hivyo ndivyo tu ulimwengu ulivyofanya.

⁶² Basi maskini mzee Samweli, alilipeleka kwa Bwana, naye akasema, “Bwana, nifanye nini kuhusu mambo haya? Watu wamedhamiria kwamba hawana budi kufanya hivyo. Na sisi—sisi hatuna budi. . . Ha—hatujui tu la kufanya juu ya hili.”

⁶³ Ndipo Bwana akasema, “Endelea moja kwa moja ukawape nanii wao—wape mfalme wao, kwa sababu hawakukatai wewe, wananikataa Mimi nisiwe Mwamuzi wao.”

⁶⁴ Mnaona, watu hawataki Roho Mtakatifu awaamue. La, la, hutaki hilo. Wanataka—wanataka kanuni fulani ya imani iwaamue, lakini, wanataka kanisa fulani liwaamue, bali hawamtaki Roho Mtakatifu.

⁶⁵ Naye akasema, “Endelea ukawafanyie mfalme.” Kwa hiyo wakatafuta-tafuta kote nchini, na huko chini katika kabila la Benyamini wakamwona mtu jina lake Kishi, ambaye alikuwa na mwana jina lake Sauli, nao wakamchagua. Mkubwa mno, mwenye sura nzuri, mwenye akili, mtu jitu, tangu kichwa hadi mabega mkubwa kuliko mtu mwingine yeyote, huko juu sana, mwenye akili, mwenye elimu, mwerevu, mwenye akili nyingi, mwenye sura nzuri. Vema, hilo ndilo hasa walilotaka, kitu ambacho wangeweza kujivunia.

⁶⁶ Hivyo karibu ndivyo makanisa yanavyofikia. Mnataka madhehebu makubwa mno, kanisa kubwa mno, zuri, kubwa kuliko ile misheni ndogo kule chini. Hivyo ndivyo tu inavyoenda. Na mara nyingi wanaondoka kwenye misheni ndogo ambako Roho anawaongoza kwenda kujiunga na hilo, kwa sababu unasema, “Mimi ni mfuasi wa Kanisa la Kwanza.” Hmm! Mnaona?

⁶⁷ Maskini ibilisi yule yule wa kale, kweli kabisa, upotovu ule ule wa watu. Kanisa lililo kubwa kuliko yote, kitu cha kujivunia, kitu fulani kikubwa. Loo, watu wanapenda kusema hivyo. Wanapenda kufikia mahali ambapo wana mchungaji aliye bora sana, mbona, wana mchungaji aliye na digrii nne kutoka Princeton ama chuo kikuu fulani mashuhuri, yeye ni mwerevu sana, na kadhalika namna hiyo. Huenda akawa na digrii hizo zote, lakini machoni pa Mungu huenda hata asitoshe kuwa mwita nguruwe. Hiyo ni kweli kabisa. Sote tu duni.

⁶⁸ Mungu, Mungu huwachagua watu, Naye ni Mfalme wetu. Mungu, Roho Mtakatifu alitumwa kuwatawala waaminio wa Kipentekoste, waaminio wa Roho Mtakatifu, yule, Mfalme Mungu, alitumwa kufanya hivyo.

⁶⁹ Sasa, wakamchagua, naye alikuwa ni mtu mashuhuri, jamaa mzuri, kile hasa walichotaka, hicho kilikuwa ni huyo jamaa. Sasa, wao, kabla hawajamtia mafuta kama mfalme, walimfanya amiri jeshi mkuu ili tu kumpa jaribio; alikuwa mshindwa, kwanza kabisa. Haikuwa katika mpango wa Mungu.

⁷⁰ Lakini hata hivyo, walipomchagua, hatimaye walikuwa wakitaka kumfanya mfalme, Samweli aliwaambia, akasema, “Sasa, endeleeni. Kwanza, kama mkichagua kuwa na mfalme na kumkataa Mungu, mnajua kitakachotukia? Hapa,” anasema, “kile kitakachotukia: Atawaita wana wenu wote na binti zenu wawe watumishi wake. Mtalipa sehemu ya kumi ya yote

mliyo nayo kulilisha jeshi lake. Na mashamba yenu mazuri ya mizabibu na wanyama wenu wote wazuri watanyakuliwa, na kila kitu. Na hivyo ndivyo itakavyokuwa. Itambidi kuwa na wabeba silaha, itambidi kuwa na askari. Binti zenu watakuwa wapishi na watengeneza vitamutamu vya kuwalisha askari. Na hivyo ndivyo itakavyokuwa.”

“Loo, hilo ni sawa, bali tunamtaka, kwa vyovyote vile. Tunamtaka, kwa vyovyote vile.”

⁷¹ Ndipo akawaita mahali fulani kabla ya kumtia mafuta Sauli awe mfalme, akasema, “Nataka kuwaulizeni jambo fulani.” Kwa maneno mengine, hebu niliweke hivi: “Je, sijawa pamoja nanyi tangu utotoni kama nabii? Je, nimewahi kuchukua yoyote ya pesa zenu? Nimewahi kuwaomba chochote?”

“La.”

“Je, nimewahi kunena nanyi katika Jina la Bwana, pasipo kutimia?”

“La, hiyo ni kweli, Samweli. Yote uliyofanya yamekuwa ni ya Bwana.”

“Vema, basi, kwa nini msimwache Mungu awe Mfalme wenu?”

⁷² “Loo, tunajua ya kwamba wewe ni nabii, tunajua ya kwamba wewe ni mtumishi wa Mungu, tunajua ya kwamba unasema kweli, nasi tunajua ya kwamba wewe ni mkweli, umekuwa mwamuzi mzuri, na kadhalika, juu yetu kupitia kwa Roho Mtakatifu, lakini bado tunamtaka mfalme.”

⁷³ Loo, ndugu, wakati watu wanapoweka vichwa vyao kwenye kitu fulani, wanaendelea tu, kwa vyovyote vile. Hakuna kitu unachoweza kufanya, wamejiamulia tu, watafanya hivyo kama ni sahihi ama si sahihi.

⁷⁴ Vema, unaweza kusimama na kuwahubiria watu kwamba ni kosa kwa wanawake wao kuvalia kizinifu, kwa wanaume kwenda, na wanawake kwenda kwenye madansi, kwenye upuuzi huu wa roki, watakimbia watoke huko nje moja kwa moja kama nguruwe kwenye kugaagaa kwake, na mbwa kwenye matapiko yake. Hiyo ni kweli kabisa. Wasilijali tena kamwe, kwa sababu wamekusudia watafanya hivyo, kwa vyovyote vile. Wanasema wanalitaka, kwa vyovyote vile.

⁷⁵ Vema. Kwa hiyo wao, baada ya maonyo yote kutolewa, ndipo hatimaye walitaka mfalme, kwa vyovyote vile, kwa hiyo Sauli alitiwa mafuta kuwa mfalme. Jambo la kwanza lililotukia, adui aliingia kisiri upande mmoja na kung’oa jicho la kulia kutoka kwa watu wengi wa Mungu. Mnajua hadithi hiyo, inapatikana hapa katika Samweli 8, 9 na 10. Akang’oa jicho lao la kulia.

⁷⁶ Hivyo ndivyo tu adui anavyotaka kufanya. Hivyo ndivyo adui anavyojaribu kufanya usiku wa leo, kuling’oa jicho la kulia la watu wa Mungu. Mliona lilikuwa ni jicho la kulia, lile lililo la

kiroho. Kama anaweza kung'oa macho ya kiroho kutoka kwenye jicho lako, ambapo unaona mambo ya kawaida na si mambo ya kiroho, amekushinda papo hapo. Mradi tu mnaweza kuwa na makanisa, na mahali pakubwa, na watu wazuri, waliovalia kiakili, na kadhalika, mradi tu jicho lako linaangalia hivyo, wala huoni upande wa roho, adui amekuweka chini ya utawala wake, maana hujui unakoenda. Amina.

⁷⁷ Ndugu, sikiliza, tunachohitaji leo ni uamsho wa kale, wa nyuma ya misitu, wa kuua dhambi, Roho Mtakatifu wa Biblia arudi kanisani tena akiwa na nguvu za Mungu juu ya kusanyiko, nao watu wamejazwa na Roho Mtakatifu. Hilo ndilo tunalohitaji leo. Na kama hilo lingetukia, kila ukuta wa tofauti za kimadhehebu ungebomolewa, wa Umoja, Uwili, Utatu, Church of God, Pilgrim Holiness, Wanazarayo, wote pamoja wangukuwa wakipaza sauti, na kula tofaa lile lile. Mbona, wange—wangukuwa wa kindugu na wa kidada sana, kusingekuwa hata na wazo moja juu yake. Lakini mnaona, tunataka kujifananisha na kitu fulani cha ulimwengu.

⁷⁸ Kitu kile kile kilichoingilia taifa letu. Taifa letu lilikuwa likitawaliwa na siasa halisi, za kweli, Wakristo wangeenda pamoja na kuomba, na kutoka wametiwa mafuta, na kujaribu kulitawala taifa letu. Sasa, limechanganyikana sana na kila kitu liwezavyo. Limepotoka! Wananiambia ya kwamba wakomunisti wako kote nchini, watu wenye mawazo huru, huku upuuzi huo wote wa kila namna wa madhehebu ukiinuka, na liko tu katika hali mbaya sana, halina kikomo. Basi inaonyesha tu jambo moja, ya kwamba Mfalme wa kweli, Mwana wa Mungu, anakuja kuchukua mamlaka na kutawala, hakika tu kama tulivyo katika mkutano huu usiku wa leo.

⁷⁹ Loo, laiti watu wangeweza tu kukumbuka, haidhuru utakaa muda gani hapa duniani, bado huna budi kukutana na Mungu. Mchukue na kumfanya Mungu kuwa Mfalme wako, Bwana wako mkuu. Watu wengi wanapenda kumpokea Yesu kama Mwokozi. “Loo, naam, sitaki kwenda kuzimuni, kwa hiyo ni—nitamchukua kama Mwokozi wangu,” bali si Bwana wako.

⁸⁰ Wakati Yeye akiwa ni Bwana, Yeye ana utawala. Anaingia moja kwa moja na kukutawala na kukuongoza. Lakini unasema, “Bwana, unaweza kuwa Mwokozi wangu, lakini usiingilie shughuli zangu za kibinafsi. Sasa, usi—usi—usiingie katika mambo *haya* yote.” Hutaki, maisha yako ya kibinafsi, hutaki kuyasalimisha yote kwa Mungu.

⁸¹ Na hiyo ni kweli, enyi marafiki. Na chochote ufanyacho utakapoondoka kwenye mkutano huu, ukiondoka kwenye mkutano huu, nenda nyumbani na azimio moja, kwamba utamtafuta Mungu, mchana na usiku na kuishi katika Uwepo Wake, uyaondokee mambo ya ulimwengu.

⁸² Loo, naam, walimtaka mfalme huyu. Basi walipompata huyo mfalme, ndipo adui akaanza kuyapofusha macho ya watu, na ndipo wasingeweza kuona mahali walipokuwa wanaenda. Hilo ndilo jambo la kwanza ibilisi analofanya wakati anapoweza kumshika mtumishi wa Mungu, humpofusha asijue kwamba amepotea.

⁸³ Hilo ndilo jambo la kwanza adui alilofanya walipomshika Samsoni, mwamuzi mwingine, waliyapofusha macho yake ambapo asingeweza kuona alikokuwa anaenda. Mara adui Mfilisti alipoivamia Israeli, waling'oa jicho lao la kulia wasiweze kuona vizuri walipokuwa wanaenda.

⁸⁴ Ninii, wakati adui anapoingia kanisani, anawapofusha macho kwenye ukweli halisi kwamba Roho Mtakatifu Ndiye anayelitawala na kuliongoza Kanisa. Nidhamu yote inaletwa na Roho Mtakatifu. Amina. Loo, laiti ningaliweza kusema maneno ambayo yangelifanya lieleweke vizuri mahali pafaapo, mnaona, hata kamwe lisiondoke, lijishikize mle ndani. Mungu alimtoa Roho Mtakatifu kulitawala na kuliongoza Kanisa, Roho Mtakatifu.

⁸⁵ Sasa, sasa, wakati jambo hili lilipotukia, waling'oa jicho lao la kulia, hivi mliona jambo hilo dogo la kijanja ambalo Sauli alifanya? Loo, alikuwa mjanja sana. Kwa sababu, alifanya nini? Alituma kote nchini, vipande vya—vya maksai ambaye alikuwa amechinja, na kusema, “Watu wote na wanifuata *mimi* na Samweli.” Loo, jamani! “*Mimi* na Samweli.” Mnaona, aliweka Samweli, akatumia sifa nzuri ya Samweli kuwadanganyia watu.

⁸⁶ Na mara nyingi siku hizi, pia viongozi wetu wanafanya jambo lile lile. Wanaliweka makanisani mwetu, wanasema, “Mbona, *Fulani-wa-fulani*, mwanzilishi wetu, aliamini, alifanya *hivi*.”

⁸⁷ Naam, alikuwa ni mtu mzuri, lakini, ndugu, jambo fulani limetukia tangu wakati huo. Hiyo ni kweli. Nini kilitukia? Ninyi Wamethodisti mliokuwa mkikaa chini ya nguvu za Mungu usiku kucha, wakati Asbury, na—na John, na Charles walipokuwa hapa Marekani, waliitwa watakatifu wanaojifingirisha, na kufukuzwa kutoka ma—makanisa halisi, makanisa makubwa. Walilala huko nje kwenye nyumba za shule, na hao watu, wangehubiri chini ya nguvu za Mungu mpaka watu wangeanguka sakafuni, nao wangeparushia maji usoni mwao na kuwapepea, huku na huku. Hiyo ni—hiyo ni... Niliwaona wakifanya hivyo.

⁸⁸ John Wesley akihubiri uponyaji wa Kiungu, kimoja cha maskini vitabu vyake, mtu mmoja kutoka kanisa la Anglikana alimwachilia mbweha na mbwa mwitu miongoni mwa kusanyiko lake, ndipo John akaelekeza kidole chake usoni mwa mtu huyo na kusema, “Jua halitatusa juu ya kichwa chako mara tatu, kabla

hujaniita nikuombee.” Jioni hiyo mtu huyo akafa kwa maumivu ya tumbo, akimwita John aje amwombee.

⁸⁹ Halafu leo hii unazungumza kuhusu ibada ya uponyaji miongoni mwa Wamethodisti? Mtu mmoja wa Kimethodisti alikuwa akiandika tasnifu kwenye kitabu papa hapa siku moja kuhusu uponyaji wa Kiungu. Akasema, “Kuna kosa moja tu ambalo Methodisti inaweza kupata kwako, Ndugu Branham.”

Nikasema, “Ni lipi hilo?”

Akasema, “Jambo moja, kwamba karibu wote wanaohudhuria mkutano wako ni Wapentekoste.”

⁹⁰ Nikasema, “Vema, tutalibadilisha tu. Ninyi Wamethodisti mnidhamini, nami nitakuja kwenu.” Nikasema, “Utalianzisha katika mji wako?”

“Vema,” akasema, “bila shaka, mimi. . .”

Nikasema, “Hivyo ndivyo nilivyowazia.” Mnaona? Hasa kabisa.

⁹¹ Mungu atatuma Ujumbe Wake mahali fulani. “Halitanirudia bure, litatimiza yale niliyokusudia. Mungu anaweza kutoka katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto.”

⁹² Lakini wanarejea kwa jamaa fulani mashuhuri, Moody, ama Wesley, ama mtu fulani mashuhuri kama huyo, walikotokea. Sasa, huo ni ujanja ule ule ambao Sauli alifanya. “Ni nani hatanifuata mimi na Samweli? Ni nani ambaye hatanifuta mimi na Samweli? Na iwe.” Vema, huo ni u—ujanja rahisi wa—wanaojaribu kuingiza.

⁹³ Lakini Samweli bado, alikuwa amewaambia watu wasifanye hivi. Lakini walifanya hivyo, kwa vyovyote vile, kwa sababu wa—walitaka kufanya hivyo, walisema wangepanya hivyo, kwa vyovyote vile.

⁹⁴ Nami nilikuwa tu nikiangalia hapa kwenye Maandiko ambapo yalisema hapa ya kwamba—ya kwamba Samweli wakati karibu awashawishi watu kwamba walikuwa wakifanya makosa, halafu wakaendelea na walitaka kufanya hivyo. Ndipo waliponinii, jambo hili lilipotukia, ndipo Sauli akapata ushindi huu, naye akatuma habari, akawaambia Waebrania wote kile walichopaswa kutarajia, kile Waebrania walikuwa wamefanya. Na kwa kweli si Sauli aliyeshinda vita, ilikuwa ni mwanawe, Yonathani, aliyeshinda vita.

⁹⁵ Ndipo tunaona, tena, ya kwamba wakati mtu huyu, Sauli, muda si muda mwajua, akawa mashuhuri basi, akatoa kifua chake, bila shaka, “Tulijenga kitu hiki kikubwa, tumefanya hivi.” Basi alipofanya hivyo, ndipo akafikia mahali ambapo hakutaka ushauri wa Samweli tena, akalifanya jinsi alivyotaka kulifanya.

⁹⁶ Na hivyo ndivyo imetendeka siku hizi. Watu wamefikia mahali ambapo hawataki kufanya jinsi Mungu anavyotaka kulifanya, wanataka kulifanya jinsi wanavyotaka kulifanya. Hiyo ndiyo shida siku hizi. Mungu anataka uponyaji wa Kiungu miongoni mwa watu Wake. Jamaa mkubwa, aliye juu anasema, “Sasa, ngoja kidogo, siku za miujiza zimepita.”

⁹⁷ Sasa, ni kitu gani kilichomfanya Sauli kufanya hivyo? Alipofika mahali ambapo alichukua uongozi wa watu, badala ya kumwacha Ro—Roho Mtakatifu . . .

⁹⁸ Sasa, Samweli alimwambia, akasema, “Sasa, kama mtaendelea na kuwa na mfalme wenu, nanyi nyote mtaishi sawa, na kuzishika amri za Mungu, na kufanya yale Bwana asemayo, na kumfuata Roho, Sauli ataweza kutuhubiria jumbe nzuri sana.” Naye alifanya hivyo.

⁹⁹ Hawakuwa na haki ya kutokumwamini Samweli, kwa sababu Samweli daima aliwatabiria kweli, aliwaambia kilicho kweli. Lakini akasema, “Sasa, kama mtamwacha tu Sauli na ninyi nyote kufuata uongozi wa Roho, mshike amri za Bwana, kila kitu kitakuwa sawa.”

¹⁰⁰ Kama hilo lingetukia usiku wa leo katika kila kanisa Marekani, kungekuwako na uamsho utakaoibuka katika taifa hili, nawaambia, vilabu vya wiski vingebomolewa, lingekuwa—lingekuwa moja ya mambo mazuri sana ambayo taifa hili limewahi kujua, kama kila mhubiri wa madhehebu yote angefuata tu uongozi wa Roho Mtakatifu, badala ya kanuni fulani za imani ya madhehebu yao, yale askofu fulani aliyosema ama mtu mwingine aliyosema, ama mtu mwingine aliyosema.

¹⁰¹ Yale mtu mwingine aliyosema hayana uhusiano wowote nalo, Mungu alimtuma Roho Mtakatifu Naye ndiye Kiongozi wetu, Yeye ndiye Kiongozi wetu. Lakini hata wanapomwona Roho Mtakatifu akitenda kazi, wanamwogopa, hawajui Yeye ni nini, ni Mgeni kwao, kwa sababu hawajafundishwa katika safu hiyo. Wanafundishwa tu juu ya jambo fulani ambalo kanisa linaamini, nao wanaendelea moja kwa moja namna hiyo, na kupitia maishani wakijiita Wakristo, na kuendelea na mambo ya ulimwengu. Ndipo wanapofikia kufa, wanasema, “Mbona, imani yangu huniokoa.”

¹⁰² Nilimwambia mtu fulani wakati fulani uliopita, nikasema, “Bwana, hivi Bwana hakukuhukumu kwa ajili ya huo uvutaji wa sigara?”

“Loo,” akasema, “la.”

Nami nikasema, “Nimekuona ukinywa pombe, mimi mwenyewe.”

Akasema, “Lakini angalia hapa, Mhubiri, nataka kukwambia jambo fulani,” nilikuwa nikimtembelea mtu mwingine chumbani, akasema, “imani yangu inaniokoa.”

¹⁰³ Nikasema, “Lakini, bwana, hebu nikwambie jambo fulani sasa, ‘Imani bila matendo imekufa.’” Kisha nikasema, “Roho Mtakatifu haishi maisha kama hayo.” Mnaona? Kisha nikasema, “Huenda ukavunjika moyo,” nikasema, “sasa, imani ni sawa, lakini kama matendo hayafuatani na hiyo imani, basi hiyo imani haifai kitu.”

¹⁰⁴ Na unapokufa, kumbuka, haibadilishi roho yako, inabadilisha tu makao yako. Na aina yoyote ya roho uliyo nayo ndani yako, hapo ndipo mahali itakapoenda, wala dhambi kamwe haiwezi kuingia Mbinguni. Kwa hiyo kama wewe. . .

¹⁰⁵ Unasema, “Vema, ninakiri yangu kila usiku. Tuna kitabu cha maombi, na tunapoenda kanisani, tunaungama dhambi zetu zote.”

Kisha mnageuka moja kwa moja na kuzifanya tena?

¹⁰⁶ Unageuka moja kwa moja kesho yake, “Mungu nisamehe kwa kunywa pombe, nisamehe kwa kufanya uzinzi, nisamehe kwa kusema uongo, nisamehe kwa kuiba,” unageuka moja kwa moja tena na kufanya jambo lile lile. “Nisamehe kwa kulewa juma lililopita, sikukusudia kunywa kiasi hicho,” unageuka moja kwa moja na kunywa tena.

¹⁰⁷ Vema, hiyo si. . . Hiyo inaonyesha ya kwamba kitu fulani hakijabadilika ndani. Unajaribu kupaka rangi upande wa nje, kidogo unapaka chokaa, bali kile kinachohitajika kufanywa ni kutiwa katika Damu ya Yesu Kristo na *kuoshwa ukawa mweupe*, badala ya *kupakwa chokaa*. Hilo—hilo ndilo u—ulimwengu unahitaji leo hii.

¹⁰⁸ Lakini basi, tunaona basi kwamba kwa sababu Sauli alijitwalia mwenyewe, Samweli alichelewa kidogo siku moja kutoa sadaka za kuteketezwa, jambo ambalo lilikuwa halali tu kwake kufanya, chini ya uvuvio wa Mungu, naye Sauli akasema, “Kwa nini tumngojee?” Alienda akaitoa mwenyewe. Akaanza kuwaongoza watu mwenyewe, badala ya kumwacha Mungu awaongoze watu. Hapo ndipo alipofanya kosa lake. Hapo ndipo kila kanisa lililopata kuunda madhehebu lingali linafanya kosa lao baya sana.

¹⁰⁹ Sijawahi kuona dhehebu, nime—nimechukua historia, nimesoma kotekote kutoka kwa *Wanzilishi Waliotangulia Nikea*, na Josephus, na wanahistoria wote wa mwanzoni, wala sijawahi kuona wakati mmoja ambapo kanisa lilipata kuingia katika uamsho mkuu, wa kiroho na kuanguka na kuuacha, ambalo liliwahi kuinuka tena. Nawatakeni mnionyeshe mahali lilipokuwa. Mungu, kama hawataifuata Nuru, Mungu ataliweka moja kwa moja kwenye rafu, na kumwacha mtu fulani, “Mungu anaweza katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto.”

¹¹⁰ Luther alikuwa ndiye Nuru ya siku zake, bali walikuwa na kundi mle ndani katika kanisa hilo la Kilutheri, nao wakayageuza Maandiko kuyafanya yalingane na theolojia yao

wenyewe, na muda si muda mwajua, kanisa la Kilutheri lilikuwa kwenye rafu, uamsho ulikuwa umekwisha.

¹¹¹ Mungu akawainua Wamethodisti. Wamethodisti wakatokea wakiwa na utakaso, walikuwa na uamsho mkuu, wa kuenea ulimwenguni, mmoja wa mikubwa kuliko yote ulimwengu uliwahi kuwa nayo katika siku za—za John Wesley, ndipo uamsho mkubwa ukaenea nchini. Kufikia wakati John, na Charles, na Asbury, na hao wote walipokufa, tuna kundi jipya mle ndani ambalo lilianza kuwazia sana kuhusu, “Vema, haitupasi kufanya *hivi*, di—dini ya Damu, na upuuzi huu wote,” ndipo muda si muda mwajua wakaanza kuingiza kila namna ya kanuni za imani, na kadhalika, na sasa angalieni mahali lilipo, limewekwa kwenye rafu. Loo, naam. Nao Wapentekoste wamefanya jambo lile lile hao walilofanya, vivyo hivyo hasa, wakifuata njia ya wote wenye mwili.

¹¹² Naam, mnataka kuwa kama ulimwengu. Msiwe kama ulimwengu, sisi ni tofauti. Watumishi wa Mungu ni tofauti, wamezaliwa mara ya pili, wao ni viumbe vipya katika Kristo. Huna haki ya kuchukua mambo ya ulimwengu na kuyachanganya na Ukristo.

¹¹³ Vazi la Kikristo halijatengenezwa kwa theolojia ya kujibunia ya kanisa, vazi la Kikristo limefanyizwa kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu wala si kitu kingine chochote, na maisha ya kufuata huo ubatizo wa Roho Mtakatifu. Yanakufanya uishi sawa, ufanye haki, utende haki, unene sawa, uishi sawa. Hiyo ni kweli.

¹¹⁴ Lakini basi wakati Sauli asingemngojea Bwana tena, Samweli alimwacha papo hapo. Kumbukeni, mara ya kwanza, si mara ya pili, lakini mara ya kwanza Sauli alipojichukulia jukumu la kuchukua utumishi wa Bwana, Samweli alimpa kisogo akamwondokea.

¹¹⁵ Na mara ya kwanza ambapo kanisa linawaruhusu viongozi wao kuchukua mamlaka ya kuwaongoza watu, Roho Mtakatifu anawaondokea papo hapo. Na mara ya kwanza kabisa unapoanza kuongozwa na mwanadamu, badala ya Mungu, Roho Mtakatifu atakuondokea, pia. Acha Roho Mtakatifu aongoze, hicho ndicho tunachohitaji ni uongozi, naye Mungu alitupa Kiongozi, nasi hatumsikii Huyu.

¹¹⁶ Hapa si muda mrefu uliopita nilikuwa nikisoma katika, Ndugu Gene aliniletea, naamini, katika moja ya magazeti kuhusu mabata bukini kuondoka Canada. Nao wana ki—kiongozi, na kama kiongozi huyu si kiongozi mzuri kweli, hawajamchagua aliye mzuri, atawapeleka popote, awapitisha njia ya mlimani, nao wote watakufa.

¹¹⁷ Hapa siku moja kundi moja liliruka, bata dume mkongwe ambaye hakujua alikokuwa akienda, hakujua mwelekeo wake, silika yake haikuwa tu sawa, aliongoza kundi la mabata bukini kote hadi Uingereza, kamwe hawajaweza kurudi. Wao—wao . . .

Asili yao ni kuhama-hama kila mwaka, nao wanakusanyika tu na kupiga makelele, na kupiga mayowe, na kuendelea huko Uingereza, wala hawajui jinsi ya kurudi nyumbani.

¹¹⁸ Inanikumbusha baadhi ya hizi nyumba rasmi, baridi, za maiti tulizo nazo siku hizi, zinaenda mbali sana na Mungu hujui jinsi ya kurudi. Kamwe hutarudi kwa kanuni za imani, huna budi kuwa na uvuvio wa kukuongoza, ndugu, na uvuvio huo huja kwa Roho Mtakatifu. Naam.

¹¹⁹ Kuongozwa na Roho, “Wana na binti za Mungu wanaongozwa na Roho wa Mungu.” Wanampenda Roho. Hawajaribu kusema, “Sasa, ngojeni kidogo, kanisa langu, hawasemi, ‘Amina.’ Kanisa langu, kamwe hawainui mikono yao, wako kimya sana. Mbona, tungemtia mchungaji wetu baridi na homa kama mtu angepiga mayowe, ‘Amina.’” Vema, unapaswa kumtia baridi mara kwa mara basi, uone tu kile kingetukia. Hiyo ni kweli. Tunachohitaji leo ni dini nzuri ya kale, ya moyoni.

¹²⁰ Hebu niwaambieni jambo fulani. Kama mtoto mchanga amezaliwa na mtoto huyo halii, hapigi kelele, hafungui maskini kinywa chake na kusema kitu, hakuna kinachotukia, mtoto huyo mchanga ana shida gani? Amezaliwa akiwa amekufa. Nafikiri tuna watoto wengi mno wanaozaliwa wafu leo, naam, kanisani.

¹²¹ Jamaa angekuja, na kusema, “Je, unamwamini Mungu, Baba Mwenyezi, Muumba wa Mbingu na nchi, Yesu Kristo, Mwanawe?”

“Naam, ninaamini.”

“Je, utaahidi kufanyia kanisa hili *hivi-na-hivi*?”

“Naam.”

¹²² Anachukua maskini chumvi yake na kutikisa na matone machache ya maji, anamfanya mshirika, anamweka kanisani. Hao ni watoto waliozaliwa wakiwa wamekufa. Naam. Hiyo ni kweli.

¹²³ Inakuwaje kwa mtoto mchanga anapozaliwa kama halii mara tu anapoanguka ardhini, kitu cha kwanza unachomfanyia ni kipi? Ni kumnyanyua, kumgeuza mkononi mwako na kumpa ninii kidogo... Unaiitaje? Unamsukuma. Hiyo ni kweli. Unampigapiga mara chache namna hiyo. [Ndugu Branham anapiga mikono yake pamoja—Mh.] Na muda si muda mwajua, “*Ng’eee!*” jinsi atakavyolia, nawe una mtoto aliye hai.

¹²⁴ Na hilo ndilo linalohitajika siku hizi kanisani, si mtu fulani aseme, “Sasa, na—najua huenda si sawa kufanya hivyo.”

¹²⁵ Maskini dondoadume wee! Unahitaji mtu nyuma ya mimbara atakayekwambia, atakayekurarua vipande-vipande, ndipo uanze kulia mara kwa mara, na kumwacha Mungu aingie, na kuruhusu jambo fulani litukie, umezaliwa basi. Si mtu anayekubembeleza kwenye dhambi zako, na kusema, “Loo,

vema, *hilo*, babu ze—zetu waliamini *hilo*.” Vema, babu zetu, Biblia yetu ilisema ni kweli; Biblia yetu ndiyo ya kweli.

¹²⁶ Ndipo Roho Mtakatifu yeye yule aliyeshuka kwenye Siku ya Pentekoste, ambapo sote tunajua ya kwamba huko kulikuwa ni kuzaliwa kwa Kanisa jipya, Roho Mtakatifu yuyo huyo asipokuletea tukio lile lile, basi una roho mtakatifu tofauti na Huyo alivyokuwa. Kweli kabisa. Kama hakufanyi uishi maisha ya kujitolea, na maisha yaliyojaa furaha na shangwe, na ubatizo wa Roho ukikuongoza katika ishara na maajabu na miujiza na kadhalika, kuna jambo fulani lililotukia. Yesu alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.”

¹²⁷ Angalieni jinsi walivyolipotosha siku hizi, wakati watu wanapoongoza: “Huyu hapa mfuasi mzuri wa kanisa. Loo, najua yeye hufanya *hivi*, loo, najua yeye hufanya *vile*. Lakini yeye ni shemasi kanisani, naye hufanya *hivi*, na *vile*, na *vinginevyo*, lakini nitawaambia, yeye bila shaka . . . unapofika wakati wa sisi kufanya mpango wetu wa kimishenari, kamwe hakosi kuweka hundi ya dola mia tano. Na kama tunafanya ukarabati, loo, yeye ni mtu mzuri!”

¹²⁸ Kisha unasimama hapo huku ukosi wako umepinduliwa na kuhubiri mazishi yake siku moja juu ya bendera nusu mlingoti, useme ameenda Mbinguni. Kitu hicho si ni dhambi? Hebu niwaambieni jambo fulani. Tunachohitaji siku hizi ni kuzaliwa upya, maisha mapya, viumbe vipya katika Kristo Yesu. Ni tofauti jinsi gani!

¹²⁹ Mtu fulani alisema si muda mrefu uliopita, mhubiri mmoja aliniambia ya kwamba ilimbidi kumchukua mshiriki fulani kanisani mwake kisiri, kasema, “Yeye ni mtu mwema, lakini,” kasema, “asingeweza kusimama mbele ya kusanyiko hilo na—na kuletwa kanisani.” Kasema, “I—ilinibidi kumpeleka kwenye chumba cha maombi huko nyuma na kumwingiza kanisani, kisiri. Kwa hiyo, unaonaje kuhusu hilo, Billy.”

¹³⁰ Nikasema, “Ningemgeuza moja kwa moja kuelekea . . . ? . . . na kumpiga teke kwa nguvu nilivyoweza. Hivyo ndivyo ningalimkaribisha ndani.” Hiyo ni kweli.

¹³¹ Nilikuwa nikishuka kwenda mtoni hapa siku moja kumbatiza mwanamke fulani, na kulikuwa na kundi zima lililokuwa likiambatana nami. Na kwa hiyo, mwanamke huyo akitembea pale, alisema, “Ndugu Branham?”

Nikasema, “Naam.”

Akasema, “Vema, hatimaye niliamua ushuke uje ukanitumbukize.”

Nikasema, “Ati nini?”

Akasema, “Uta—utaniandaa alasiri ya leo, unitumbukize, sivyo?”

¹³² Nikasema, “La, mama. Kabla sijafanya hivyo,” nikasema, “huna budi kuupatanisha moyo wako na Mungu, nisingekubatiza kwa vyovyote vile, ungali hai ulimwenguni bado. Huna budi kufa, tunawazika tu watu waliokufa, wale waliokufa katika Kristo, na wako tayari kufufuka kwenye maisha mapya tena.” Basi mtu anayetoea tamshi kama hilo dhidi ya ubatizo hafai kwa ubatizo wa maji. Sawa.

¹³³ Vema, huko ndiko tuendako. Tunaona roho . . . Sauli alisema, “Nitafanya hivyo mimi mwenyewe, najua jinsi ya kulifanya, najua mengi kulihusu kama yule mzee asiyelewa, Samweli.”

¹³⁴ Naye Samweli alikuwa amethibitisha ya kwamba alikuwa ni mtumishi wa Mungu, alithibitisha ya kwamba Roho Mtakatifu alikuwa pamoja naye, kwa kuwa alisema, “Nitawashuhudia leo hii: Nimewahi kusema nanyi lolote katika Jina la Bwana pasipo kutimia? Hivi nimewahi kuja, nikawasihi na kuwaombaomba pesa na mambo haya yote makuu?”

¹³⁵ “La,” wakasema, “hujafanya hivyo, bali hata hivyo sisi—sisi tunataka kufanya tutakavyo, mnaona.” Na hiyo ni, ndipo mnaona kile walichokuwa wakipata basi.

¹³⁶ Sasa, tunaona basi, mtu anapokataa uongozi wa Roho Mtakatifu, mnajua kile Mungu alimfanyia Sauli? Alimpa pepo mchafu amwongoze. Sasa, vipi kuhusu hilo? Alimpa pepo mchafu, Mungu alimpa pepo mchafu amwongoze. Kwa hiyo mtu anapokataa uongozi wa Roho Mtakatifu, au mtu yeyote anapokataa uongozi wa Roho Mtakatifu, unaye ibilisi juu yako wa kukuongoza. Hiyo ni Biblia hasa.

¹³⁷ Ee Mungu, laiti tungekuwa na uamsho. Laiti ungaliweza kuja wakati ambapo Roho Mtakatifu kweli angeweza kuingia moyoni mwa Wamarekani tena, ambapo wanguweza kuona kwamba ni Yeye. Wanataka kuangalia, waseme, “Vema, sasa angalia, siwezi kushiriki katika mkutano huu kwa sababu kanisa langu halininii. . .”

¹³⁸ Hiyo inaleta tofauti gani? Hilo lina uhusiano gani nalo?

¹³⁹ “Vema, nitakwambia, wao—wao wanaamini *hili*, nasi hatuamini lile.”

¹⁴⁰ Mradi tu wanahubiri Biblia, na Biblia nzima, na Injili yote, na ukweli mtupu, usikieni, mradi tu wanaongozwa na Roho, aminini, naye Mungu atajitambulisha Mwenyewe. Kama mtu anaongozwa na Roho wa Mungu, Mungu atajitambulisha Mwenyewe kwa mtu huyo. Naam, bwana. Mungu aliahidi kufanya hivyo. Kwa hiyo katika kufanya hivyo, tunajua basi ya kwamba—ya kwamba Roho Mtakatifu huwaongoza watu na Mungu hulishughulikia. Amina. Unaamini hilo kwa moyo wako wote? Bila shaka, tunaamini. Vema.

¹⁴¹ Basi ningetaka kusema jambo lingine: Roho huyo mchafu alianza kumwongoza Sauli, naye akamwongoza; na leo hii

wakati Roho Mtakatifu anapokataliwa, anataka, Yeye... Atafanya nini? Utapata pepo mchafu wa kukuongoza.

¹⁴² Sasa sikilizeni, sitaki kuwaudhi, bali nataka mpate jambo hili. Mnaona? Kama tu ilivyokuwa katika siku hizo, ndivyo ilivyo siku hizi. Hawataki Roho Mtakatifu awaongoze, kwa hiyo wanapata pepo mchafu. Ni kitu gani kinachotukia kwa pepo mchafu? Pepo mchafu, anataka kuongoza—anataka kuwaongoza basi. Na sasa nini? Wao hawataki, hawakutaka Mungu awe Mwamuzi wao; wala watu siku hizi hawataki Roho Mtakatifu awaamue. Hiyo ndiyo sababu walimkataa Samweli, kwa sababu hukumu yake ilikuwa ni ya Mungu, ilikuwa ni ya Kimaandiko, wala hawakutaka kuongozwa na Roho, nao wakamkataa wamchukue mtu wa kikanisa. Nao walipata nini? Pepo mchafu wa kuwaongoza.

¹⁴³ Sasa, watu siku hizi hawataki kuongozwa na Roho Mtakatifu, hawataki Roho Mtakatifu awaamue. Sasa, hiyo ni kweli, enyi marafiki. Hawataki Roho Mtakatifu awaamue.

¹⁴⁴ Ndipo watu wakaniambia, mwanamke mmoja aliniambia si muda mrefu uliopita, nilikuwa nikihubiri kwa nguvu sana, nami nilikuwa nikiwakemea akina dada kwa kukata nywele zao, na kuwaambia ya kwamba Biblia ilisema alikuwa ni kahaba kama angefanya hivyo, alikuwa—alikuwa si mwaminifu kwa mumewe, naye mume alikuwa na haki ya kumwacha. Hivyo ndivyo Maandiko yasemavyo hasa. Mwanamke yeyote atakayekata nywele zake kutoka kichwani mwake, anamwaibisha mumewe, Biblia ilisema, ambaye ndiye kichwa chake. Nawe unaweza kuwahubiria... Mama huyo alikutana nami nje, naye akasema, “Hebu nikwambie jambo fulani sasa hivi, Mhubiri! Hakika utaiharibu huduma yako!”

Nikasema, “Huduma yoyote ambayo Neno la Mungu litaharibu, inapaswa kuharibiwa.” Hiyo ni kweli kabisa.

Akasema, “Vema,” akasema, “kila mtu ataondoka na kukuacha.”

Nikasema, “Mradi tu Yeye anakaa pamoja nami, hilo ndilo jambo muhimu, unaona, kumwacha Yeye akae.”

¹⁴⁵ Na, hakika hawataki, hao watu... Huninii... Kwa sababu wanataka kuwa kama walimwengu. Hawataki, wanawake hawataki kuva kama watu wa Mungu, wenye heshima, wenye maadili. Mbona, hapa majuma machache yaliyopita, nilihudhuria mkutano wa Kipentekoste. Sasa, ninyi Wabaptisti jitayarisheni kupaza sauti, na Wapresbiteri. Nilienda kwenye moja ya makanisa mashuhuri sana ya Kipentekoste ya Marekani, nami na mwenzangu tulikuwa tumeketi pale, nilikuwa niwe na ibada ya Jumapili asubuhi.

¹⁴⁶ Ndipo wakati... Walijua ya kwamba sikuzote ninapinga upuuzi kama huo, ndipo basi walipoachilia shule ya Jumapili, nilikuwa nimeketi pale kwenye eneo la kuegeshea magari, hawa

hapa walimu wa shule ya Jumapili wanakuja, la, sasa, hao si—hao si Wamethodisti, hao ni Wapentekoste, nywele fupi sana, zilizokatwa, na vipodozi usoni mwao mwote, ilionekana kana kwamba walikuwa wakila mnofu mwekundu wa nyama ya ng'ombe, wakautia kote kwenye kucha zao za vidole, na—na kote nje namna hiyo, rangi hiyo yote na rangi ya makucha, wakitembea huko nje, na hawa hapa wanaume wa rika langu wanakuja wakiwa na mtindo huo wa kukata nywele kitofali na wenye mikia ya bata mgongoni namna hiyo.

¹⁴⁷ Ndugu, kama ningekuwa na kusanyiko kama hilo, hakika ningewararua vipande-vipande, ndugu, hakika ingekuwa. Naam, bwana.

¹⁴⁸ Loo, hawakutaka kukaa na kumsikiliza mtakatifu anayejibingirisha akihubiri. Halafu wanadai kuwa ni Wapentekoste! Bwana aturehemu! Nikapanda kule, ndipo mwalimu wa shule ya Jumapili akatokea, akasema, “Habari za asubuhi, Kasisi Branham,” na huo wote, upuuzi huo wote mwekundu usoni, na penseli hii nyeusi juu ya macho yao, na—na yote—yote hayo, na kuvalia kizinifu sana.

¹⁴⁹ Nao wanasema, “Vema, sasa ngoja kidogo. Ndugu Branham, hiyo ndiyo aina pekee ya nguo unazoweza kununua.”

¹⁵⁰ Wangali wanauza vitambaa na cherehani, kwa hiyo hamna—hamna udhuru hata kidogo. Hiyo ni kweli. Kama unaongozwa na Roho Mtakatifu, jinyoshe.

¹⁵¹ Hawataki Roho Mtakatifu awaamue. Hawataki. . . Hakuna udhuru, Mungu hatasikiliza udhuru wenu. Asingesikiliza wa Sauli, wala Yeye hatakusikiliza. Huna budi kufanana na yale Biblia iliyosema.

¹⁵² Nafikiri mwanamke yeyote anapaswa kuwa safi, anapaswa kuonekana nadhifu awezavyo, mwanamume yeyote anapaswa, pia, kuonekane mtanashati na safi, lakini awe na adabu. Unajua kama ukivaa tu maskini nguo hizo ambazo watu huvaa, maskini kaptura hizo na. . . Mwanamke aliniambia wakati fulani uliopita, kasema, “Ndugu Branham, mimi sivai hizo kaptura,” kasema, “Mimi huvaa suruali ndefu.”

Nikasema, “Hizo ni mbaya zaidi, hizo ni mbaya zaidi.”

¹⁵³ Mnajua aliyosema Mungu? “Ni chukizo machoni pa Mungu kwa mwanamke kuvaa vazi limpasalo mwanamume.” Naye Mungu ni Mungu wala kamwe habadiliki, Yeye ni Mungu asiye na kikomo. Kama wakati mmoja ilifanya uvundo unaochefua na kutoa harufu mbaya mbele Zake, bado inatoa uvundo na harufu mbaya inayochefua kumwona mwanamke akivaa vazi limpasalo mwanamume. Aliwafanya wanaume, *wanaume*, na kuwafanya wanawake. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . kama halihubiri hivyo. Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema. Ni kweli kabisa. Loo, hawataki hilo.

154 Mama mmoja aliniambia, kasema, “Vema, unafikiri ni vibaya kwa mwanamke kujipodoa, vipodozi hivi?”

155 Nikasema, “Naam, bwana, nafikiri.” Nikasema, “Kabiliana...Mungu kamwe...Kama angalitaka uonekane kama kwamba ulikuwa kibanda, Yeye angekufanya kibanda,” nikasema, “kilichopakwa rangi namna hiyo.” Kama alitaka uvute sigara, angeweka bomba la moshi juu yako, na dohani kadhaa upate kuutolea. Lakini Yeye—Yeye alikupa mapafu ya kupumulia hewa nzuri, safi, hiyo ndiyo sababu ya Yeye kufanya hivyo.

156 Lakini wao, loo, la, bali ninyi...Hawamtaki yeyote, hawataki Roho Mtakatifu awahukumu. Sasa, kama ukimpokea Roho Mtakatifu na bado unaweza kuishi hivyo, unijie uniambie ati una Roho Mtakatifu na unaishi hivyo, si—siwezi kuwa hakimu wako, lakini kulingana na Neno umeenda kombo mahali fulani, ndugu. Hiyo ni kweli. Hivyo ndivyo hasa Roho asemavyo. Mnaona? Hiyo ni kweli. Tunahitaji utakatifu urudi tena, ndugu. Tunahitaji: Kumrudia Mungu.

157 Naam, wanamkataa, bila shaka wanamkataa. Hawataki kujua jinsi ambavyo...Hawataki kutiishwa na Roho Mtakatifu, hawataki Roho awaongoze.

158 Hebu niwaambie jambo fulani, enyi kina mama, siwadhihaki, hapa si mahali pa jambo hilo, hapa ni mahali ambapo hukumu inatolewa. Nayohukumu haina budi kuwa ya haki, na hukumu ni kwa Neno la Mungu. Angalieni, kulikuwa na mwanamke mmoja tu katika Biblia nzima aliyewahi kujipaka rangi usoni, hiyo ni kweli, mwanamke mmoja. Wala hakujipaka rangi uso wake akakutane na Mungu, alijipaka rangi usoni apate kukutana na mwanamume apate kumshawishi, hiyo ni kweli, Yehu. Yezebeli, mnajua yale Mungu aliyomfanyia? Alimlisha kwa mbwa. Hiyo ni kweli.

159 Kwa hiyo unapomwona mwanamke aliyejipodoa, sema, “Huyo ni Binti Nyama ya Mbwa.” Hivyo ndivyo ilivyo hasa mbele za Mungu, Yeye alimlisha mbwa. Kwa hiyo hao tu ndio aliowafaa walikuwa ni mbwa. Alimlisha mbwa. Ni wangepi wanaojua hiyo ni kweli? Semeni, “Amina.” Hiyo ni kweli kabisa.

160 Kwa hiyo mnaona, jinsi tabia hizo za kikafiri zinavyoingia kanisani, ni kwa sababu mwana fulani vuguvugu wa Kishi husimama nyuma ya mimbara na anahofia tiketi yake ya posho kuhubiri ukweli. Ndugu, hebu nikwambie, tunahitaji wanaume nyuma ya mimbara, wala si kundi la dondoadume wa kitheolojia wanaoogopa kitu cha kuwaambia watu. Tunahitaji watu hodari, watu wazuri, waliojazwa na Roho Mtakatifu, wanaosimama hapo ambao hawatahubiri upuuzi wa dondoadume, na kanuni za imani, na madhehebu, bali watahubiri Injili, na kuwabambua ngozi. Hiyo ni kweli kabisa. Kweli.

¹⁶¹ Maskini mtoto wako, ati useme, “Sasa, Kadogoo, kipenzi, usifanye hivyo.” Chukua kijiti ukamchune ngozi. Hicho ndicho unachohitaji. Angalieni kile mlicholea kutoka kwenye hiyo “Kadogoo, mpenzi.” Mtoto Martha, mwajua, ataichapua miguu yake na kumwambia mama yake, “Wewe funga domo, sitafanya hilo!” Loo, jamani! Ni vema hawakuwa na baba yangu. Hiyo ni kweli. Naam, bwana.

¹⁶² Upuuzi huu wote, mnaona mlichochacho? Kundi la baradhuli vijana. Kile hasa mlichochacho. Kichaa, hasa kabisa. Hospitali za wendawazimu zinajaa. Wahuni, hiyo ndiyo iliyosababisha hayo, “Kadogoo, kipenzi.” Biblia ilisema usipotumia fimbo, unamharibu mwanao. Hiyo ni kweli kabisa.

¹⁶³ Na Mungu anajua ukweli ni upi na yaliyo bora zaidi. Samweli alijaribu kumwambia Sauli hivyo. Mungu alijua kilicho bora zaidi, lakini Sauli akasema, “Vema, watu wananitaka.” Hilo—hilo ndilo. Mradi tu anapata mtu wa kumfuata, hilo tu ndilo alilotaka. Alitumia jina la Samweli, apate mtu wa kumfuata, hilo tu ndilo alilotaka.

¹⁶⁴ La, hawataki hiyo Injili halisi, ya kweli, hawataki kweli ile halisi, hawataki Roho Mtakatifu ku—kuwaongoza. Afadhali wawe na mchungaji wa kiakili. Mnaona? Sasa, huyu hapa aina ya mtu wanayemtaka, mtu fulani. . . hawataki. . . wanataka mtu ambaye hatawaambia ni kosa kufanya *hili*, na ni kosa kufanya *lile*, na kuacha kufanya *hili*, na kuacha kufanya *lile*. La, hawataki hilo.

¹⁶⁵ Lakini wanataka mtu aliye na ujuzi wa kitheolojia, wa seminari, ambaye wanaweza kusema ana digrii kadhaa, naye anasimama vizuri sana, na anavaa nadhifu sana, ambayo ni sawa kabisa. Lakini anapofika pale kwa namna fulani hufanya tafsiri yao wenyewe ya Biblia ya, si kulingana na Biblia, bali kulingana na ujuzi fulani wa seminari ya kitheolojia, badala ya ubatizo wa Roho Mtakatifu chini ndani yake kumfanya abambue ngozi. Hiyo ni kweli kabisa.

¹⁶⁶ Niambie nabii katika Biblia, ambaye alikuwa ni nabii wa kweli, ambaye hakuwachuna ngozi, niambie moja lililowahi kutimia. Wala hawakutaka kuwaamini wakati huo, bali Mungu aliwapa ishara na maajabu kuwafuata ili kuwafanya watu, kuthibitisha ya kwamba huduma yao ilikuwa sahihi. Daima imekuwa hivyo.

¹⁶⁷ Roho Mtakatifu, leo hii, anashuka moja kwa moja Kanisani, na kusema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: Katika Jina Langu watatoa pepo, watasema kwa lugha mpya, watashika nyoka, ama kunywa kitu cha kufisha; wataweka mikono juu ya wagonjwa, nao watapata afya.

¹⁶⁸ “Siku ya Pentekoste ilipotimia, wote walikuwa mahali pamoja na moyo mmoja. Mara kukaja uvumi kutoka Mbinguni kama upepo wenye nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote

waliyokuwa wameketi. Ndimi zilizogawanyika zikawakalia, kama za moto. Wote wakajazwa na Roho Mtakatifu, wakaanza kunena kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka.”

¹⁶⁹ Hao wakaenda mitaani wakipiga mayowe, na kucheza dansi, na kutenda kama walevi, kama tu... Basi kumbukeni, ninyi Wakatoliki, bikira Mariamu mbarikiwa alikuwa miongoni mwao. Na kama asingeweza kwenda Mbinguni bila kupata tukio la namna hiyo, utawezaje wewe? Unaona? Wazia jambo hilo. Naam, bwana. Huyu hapo alikuwa amejaa Roho Mtakatifu kana kwamba walikuwa wamelewa, wanaume na wanawake wote pamoja. Chochote pungufu ya hayo, umepungukiwa na Pentekoste.

¹⁷⁰ Sasa, wanafanya nini siku hizi? Wanakuchukua, wanakuletea maskini barua zilizochakaa kutoka kwa makanisa manne ama matano mbalimbali ambayo yamekuwa nayo, na kuiweka hapo chini, na kukuweka kanisani, na kukuita mfuasi. Loo, huyo hapo Sauli, unaona, hivyo ndivyo alivyofanya hasa. Lakini Samweli alitaka kuongozwa na Mungu.

¹⁷¹ Watu hawa huenda kanisani Jumapili asubuhi, mchungaji kulifasiri Neno, wanarudi moja kwa moja huko nje, na kufanya watakalo juma zima. Anawaambia, wanaenda nyumbani akisha kuwapa tafsiri ya mambo machache ya kanisa, nao wanakariri kanuni chache za imani, wanaenda nyumbani kidogo wameridhika, wakijifariji wenyewe, “Dini yangu yote imefanywa. Ni sawa mpaka juma lijalo, nitashuka niende tena. Wanakula ushirika Jumapili asubuhi, mkate na maji ya zabibu,” na kadhalika, na lolote wafanyalo, na kuliacha liendelee namna hiyo. Loo, ndugu! Hmm!

¹⁷² Lakini sasa, Sauli alifanya nini? Hakika aliunda jeshi kubwa, bila shaka aliliunda, akawaingiza Israeli kwenye jeshi kubwa. Aliwafanya wote pamoja na mikuki mizuri, iliyong’arishwa. Aliwafundisha kwa mikuki hiyo kupigana kama tu, kama watu halisi, hodari, aliwatengenezea wote ngao kubwa, na kadhalika. Wote waliadibishwa kabisa na kufunzwa vilivyo mpaka dakika ya mwisho.

¹⁷³ Vema, walikuwa wanaendelea vizuri. Mataifa mengine yaliangalia huko nje, kasema, “Mnajua, Israeli inapiga hatua vizuri sana.” Lakini siku moja, siku moja, Mungu haliachi liendelee muda mrefu sana, mpaka siku moja akaja mpinzani jina lake Goliathi, akakunja mikono yake, nao Israeli wakatetemeka mpaka viatu vyao vikatetemeka ardhini. Maskini huyo mtu tangu-bega-hata-kichwa-mrefu-kuliko-hao-wengine-wote akatetemeka pamoja nao, pia, huyo hapo amesimama, hajawahi kuona kitu kama hicho. Ilibidi Roho achukue mamlaka, ilimbidi Mungu wa Israeli aonyeshe nguvu Zake. Loo, naam.

¹⁷⁴ Kutakuwako na Goliathi mahali fulani. Tumekuwa na mmoja si muda mrefu uliopita. Tuna wengine siku hizi, sielewi ni kwa nini. Tuna watu wenye akili nyingi zaidi, umati uliovalia vizuri kuliko wote, tuna seminari zilizo bora sana za kitheolojia, baadhi ya watu waliofunzwa vizuri sana waliowahi kutoka nje, wamezifundisha kwaya hata zinaweza kuimba *Jinsi Wewe Ulivyo Mkuu* mpaka ni vigumu kwa Malaika Wakuu kujilinganisha nao. Loo, wamefunzwa katika shule zilizo bora zaidi, na kila kitu namna hiyo, wakijua yote kulihusu, lakini inapofikia wakati wa mambo ya Kimbinguni, hawajui lolote kuyahusu.

¹⁷⁵ Mungu alimtuma mpinzani huko kuonyesha ni yupi alikuwa sahihi, kuonyesha ya kwamba kitu hicho hakikuwa sahihi. Na ndugu, nasema hili kwa upendo na heshima ya kiungu: Mmoja wa wana wetu wa Kishi, tangu mabega hata kichwa mrefu kuliko wainjilisti wengine wote, aliitwa na Mwislamu hivi majuzi, na kupewa changamoto kwa Neno la Mungu, ndipo akatetemeka kwenye viatu vyake, na kuondoka mahali hapo. Loo, jamani! Kuna nini? Ilikuwa ni kitu fulani mbali na theolojia, ingelimbidi kuleta nguvu za kimbinguni za Mungu na kufanya hivyo, hakujua lolote kulihusu. Ndivyo ilivyokuwa katika siku za Sauli.

¹⁷⁶ Lakini sikilizeni, ninyi waaminio wa kweli katika Kristo, ninyi Wakristo wa kweli mnaomwamini Mungu na mambo ya kimbinguni, wakati wote Sauli alipokuwa akilifundisha jeshi hili kubwa, na wasomi hawa wote wakija, Mungu alikuwa na maskini Daudi huko nje mahali fulani akiwalisha kondoo wa baba yake Chakula cha kondoo, Neno, si magugu ya kitheolojia. Kweli. Ilitokea kwamba alikuwa amesimama karibu wakati jambo hilo lilipotukia. Loo, jamani!

¹⁷⁷ Walitaka kumpa ujuzi wa seminari, Sauli akasema, “Njoo hapa, labda silaha zangu zingekutosha.”

Akasema, “Niondoleeni kitu hicho.”

“Vema, nitakufanyia Shahada ya Sanaa na kukupa digrii ya Udaktari.”

¹⁷⁸ Akasema, “Sijui lolote kuihusu, niondolee kitu hicho. Lakini hebu niwaambie jambo fulani, nina kombeo hili.”

“Vema, hilo lisingelinganishwa . . .”

¹⁷⁹ “Lakini angalia hapa, siku moja mwana-kondoo alikuwa huko nje akila, mmoja wa kondoo wa baba yangu alikuwa huko nje akila, ndipo simba akaingia na kumkamata, akatoroka naye. Ndipo nikachukua kombeo hili, nami nikamtumainia Mungu wa Israeli, nami nikamfuatilia, na kumwangusha chini, na kumwua, na kumrudisha huyo mwana-kondoo.”

¹⁸⁰ Kasema, “Dubu akaingia na kumchukua mwana mbuzi na kuanza kwenda naye, mmoja wa wa baba yangu, ndipo nikaweka jiwe katika kombeo, na ni kitu kidogo sana, lakini ni—

nilimfuatilia. Sikuwa nikitumainia hilo kombeo, bali nilikuwa nikitumainia nguvu za Mungu wa Israeli.” Amina.

¹⁸¹ Ni kitu gani hicho? I-m-a-n-i k-a-t-i-k-a Y-e-s-u. Hiyo ni kweli. Kutumainia nguvu za Mungu wa Israeli. “Nami nikamwangusha chini huyo dubu, nikamtoa yule simba... maskini yule kondoo kutoka kinywani mwake, na kumrudisha.” Akasema, “Na ni zaidi sana vipi... Mimi—mimi ni mhudumu wa ukombozi, ninajua ninalozungumzia.”

¹⁸² Sikilizeni, wana maskini Daudi wengine wadogo ulimwenguni siku hizi, hawa—hawatambuliwi na Sauli, hiyo ni kweli, lakini kuna maskini Daudi wengine wadogo ulimwenguni wanaowachunga na kuwalisha kondoo wa Mungu, Chakula cha kondoo. Ndipo siku moja kansa kubwa mno ikaingia na kumshika mmoja, daktari akasema, “Vema, ameisha.”

¹⁸³ Lakini maskini Daudi huyo mdogo akasema, “Sijui, sina mengi sana, maombi tu ya imani, bali ninakufuatilia, kwa sababu wewe ni kondoo wa Baba yangu. Nina imani.” Haleluya! “Ninakufuatilia.”

¹⁸⁴ Kulikuwa na kiharusi cha kupooza kilichompata mmoja, akasema, “Sijui nitampataje, lakini ninakufuatilia, wewe ni mmoja wa kondoo wa Baba yangu.” Haleluya! Usimkatae Mfalme wa Israeli. Utukufu! Whiu!...?...

¹⁸⁵ Hakuwa na mengi sana, bali alikuwa na imani katika Mungu wa Israeli. Nawaambia, walikuwa wamekataa, walikuwa na kwaya zao zote, na wasomi waliofunzwa, na theolojia, lakini ilipofikia mambo ya kimbinguni, walikuwa wamedumaa, hawakujua chochote juu yake. Kwa nini Daudi hakumjua mtu huyu shujaa? Kwa sababu alikuwa akila katika malisho mengine. Hiyo ni kweli. Alikuwa akifanya mazoezi chini ya mazingira mengine.

¹⁸⁶ Siku moja u—ugonjwa uliingia na kumshika mmoja wa kondoo wa Baba na ungempeleka kwenye kaburi la mapema. Maskini hawa Daudi wadogo walisema, “Sijui jinsi nitakavyofanya hilo.”

Wakasema, “Aa, upuuzi, maskini kombeo hilo.”

¹⁸⁷ “Huenda nisijue jinsi ya kulifanya, bali ni ahadi, nami nina imani nalo, kwa hiyo ninamfuatilia mwana-kondoo huyo.” Naye akamrudisha. Haleluya! Loo, jamani! Tunachohitaji usiku wa leo ni kuondoka kwenye theolojia hii yote ya kujibunia, na kumrudisha Mfalme, na imani katika Mwana wa Mungu...?... upuuzi huu wote. Naam, bwana. Msijali.

¹⁸⁸ Waliogopa kuutangaza ule mkutano huko Afrika Kusini. Joseph Boze alifanya hivyo. Wakati Waislamu elfu kumi walipoketi kule na kumwona maskini mvulana mdogo aliyepinda namna hiyo, akiyumbayumba jukwaani hata hana akili timamu, lakini walipomwona Roho Mtakatifu akimwambia

yeye alikuwa ni nani, kilichotukia, na kilichokisababisha, ndipo alipomaliza kuomba, alinyooka moja kwa moja kama mwanadamu namna hiyo, Waislamu elfu kumi waliweka nyara zao chini na kumkubali Yesu Kristo kama Mwokozi binafsi. Naam, bwana.

¹⁸⁹ Waangalieni Tommy Osborn, Oral Roberts, watu wanaolisha kundi kwa Chakula cha kondoo. Siku za miujiza hazijapita, kama wasemavyo wanatheolojia. Kama siku za miujiza zimepita, siku ya Mungu imepita; Mungu ni mwujiza, bila shaka. Haya basi, Chakula cha kondoo.

¹⁹⁰ Loo, maskini rafiki yangu, mwenye huzuni, huenda ibilisi alikupeleka, dada, huko nje mahali ambapo kamwe hutamani kuacha nywele zako zikue, huenda akakufikisha mahali ambapo unafikiri ya kwamba mchungaji fulani ni upuuzi wakati anapokuhubiria utakatifu safi, jinsi mnavyopaswa kuvalia, baadhi yenu wanaume huko nje mnaoenda huku na huko na kufanya mambo haya msiyopaswa kufanya.

¹⁹¹ Nanyi wanaume ambao utamwacha mke wako afanye jambo kama hilo, na kuvuta sigara, nina heshima duni kwako angalau kama mwanamume. Sasa, hiyo ni kweli kabisa. Mwajua, mwanamume ndiye kichwa cha nyumba, mradi tu anachukua mahali pake. Lakini sisi... Mimi—mimi sininii... Ninapenda kumwona mwanamume aliyeye *mwanamume*. Mwanamume hapimwi kwa misuli mingapi aliyeye nayo, huyo ni mnyama, mwanamume hapimwi kwa misuli migumu, bali hupimwa kwa makovu yaliyo kwenye magoti ya suruali yake, ambapo amekuwa akiomba. Hilo ndilo linalomfanya mwanamume.

¹⁹² *Mwanamume* ni tabia, si unyama, bali tabia. Nimewaona wanaume wenye uzito wa ratili mia mbili, wasiokuwa na wakia moja ya *mwanamume* ndani yake, akimnyakua mtoto mchanga kutoka mikononi mwa mama yake na kumnajisi. Mwanamume yeyote ambaye angempa mwanamke sigara ni duni na ni bure; na tukijua ya kwamba huyo ni mmoja wa vibaraka wakuu sana wanaovunja uti wa mgongo wa taifa letu.

¹⁹³ Na viwanda hivi vya sigara, na kadhalika hapa nje, vikisambaza sigara na wiski, na—na halafu wanachukua na kufutilia mbali kodi yote ya mapato kwa matangazo haya kuweka uozo zaidi kwenye televisheni, na kuwaiga wanawake hawa... Ee, Mungu, nchi yetu ina shida gani? Imeukataa uongozi wa Roho Mtakatifu, ambao haungevumilia hata kidogo mambo kama hayo. Si ajabu maradhi na magonjwa yameenea sana. Tunachohitaji siku hizi ni Mungu, Mfalme aliyekataliwa, Mfalme wa Israeli kutembea miongoni mwetu namna hii.

¹⁹⁴ Huenda alikuchukua namna hiyo. Huenda kukawa na wagonjwa hapa usiku wa leo watakaosimama kwenye mstari huu wa maombi, huenda wakasimama hapa, huenda kansa imekuvamia, huenda ibilisi alikupeleka mbali usikoweza

kufikiwa na daktari, daktari wako mpendwa, naye amekupeleka mahali ambapo huwezi kurudi.

¹⁹⁵ Hiyo inaweza kuwa hivyo, lakini hebu nikwambie jambo fulani, ndugu, ninapowaleta kwenye mstari huu wa maombi usiku wa leo, sina kitu ila kombeo dogo linaloitwa i-m-a-n-i, ninakufuatilia. Hiyo ni kweli. Nakufuatilia, nimemwona akiwarudisha wengine, atakurudisha, pia. Naam, bwana. Mungu ambaye angeweza kuwaponya watu hawa, watu wengine, anaweza kukuponya. Unaamini hilo? Naam, kweli.

¹⁹⁶ Mungu yeye yule angali hai, nasi tunamfuatilia usiku wa leo, na kwa nguvu na imani katika Yesu Kristo tutamwangusha huyo ibilisi chini kabisa, na kumrudisha. Ni kwa nini? Ni kondoo wa Baba, ni maskini mwana-kondoo wa Mungu ambaye Shetani alimwiba, na kusema, “Ah, ana ushawishi mwingi, nitamtoa kanisani. Nitamtoa kanisani.” Njoo, Daudi, hima twende! Naam, bwana. Mungu alituahidi ushindi, ni zaidi sana vipi huyu Mfilisti asiyetahiriwa, asiyeamini atasimama na kulitukana Neno la Mungu aliye hai! Naam bwana.

¹⁹⁷ Nitakuwa kama wale wana wa Kiebrania, “Mungu wetu aweza kutukomboza, lakini hata hivyo, hatutazisujudia sanamu zozote,” za madhehebu rasmi wala chochote kile. Nitakuja, hivyo tu ndivyo ninavyoweza kufanya. Siwezi kusema ninaweza kumrudisha, bali ninakuja, nikijaribu. Nitakabiliana naye katika Jina la Yesu Kristo nikiwa na agizo la Malaika aliyenijia, na kusema, “Kama utawafanya watu wakuamini, na uwe mwaminifu unapoomba, hakuna kitu kitakachosimama mbele ya maombi yako.”

¹⁹⁸ Imefanywa kwa makumi ya maelfu mara maelfu. Enyi maskini kondoo wadogo wagonjwa usiku wa leo, ninawafuata sasa, katika Jina la Yesu Kristo. Na—nataka kuwarudisha, mbali na sehemu hizo za kale kwenye malisho ya kijani kibichi yenye kivuli na maji matulivu, ambapo unaweza kulala chini na kuweka unyasi kinywani mwako na kumwangalia Mungu, useme, “Loo, nina amani kama mto, nina amani kama mto.” Naam, hivyo ndivyo tunavyotaka kufanya.

¹⁹⁹ Loo kuna zaidi, kuna wachungaji. Ni wahubiri wangapi humu ndani wanaoamini katika ukombozi wa—wa wagonjwa na wanaoteseka? Angalieni tu hapa. Unarudi, maskini mwana-kondoo, usiku wa leo, maana tunakufuatilia. Naam, bwana. Ibilisi huyo simba anayeitwa kansa, huyo ibilisi simba aitwaye chochote anachotaka kuitwa kwa jina la matibabu, chochote alichu, yeye ni ibilisi, nasi tuna agizo kutoka kwa Yesu Kristo, “Katika Jina Langu watatoa pepo.” Afadhali aanze kwenda, maana kuna kuni hapa, nasi tutamkamata usiku wa leo, tunakuja kuwarudisha.

²⁰⁰ Ni wangapi walio na hizo kadi za maombi sasa? Inueni mikono yenu. Billy yuko wapi? Ingia hapa ndani, popote alipo,

Billy Paul, baadhi yenu. Ninawatakeni ninyi mlio na kadi za maombi msimame papa hapa chini. Jipangeni sawasawa kabisa jinsi mliyokuwa jana usiku. Wale tu walio na kadi za maombi kwanza, tafadhalini, walio na kadi za maombi, hapa. Vema.

[Ndugu mmoja ananena kwa lugha, ndugu mwingine anafasiri—Mh.] Amina.

²⁰¹ Njoo, ukiamini, kuwa na imani. Yako ilikuwa umbali gani huko chini mstarini, dada? Hiyo ni kweli. Panga mstari wako wa maombi. (. . . ? . . .)

²⁰² Wakati mmoja, Daudi . . . Sasa, ninyi tu mlio na kadi mliokuwa hapa jana usiku. Sininii. . . Hawakugawa zozote usiku wa leo, tutazigawa tena kesho jioni. Ninyi mlio na kadi simameni hapa kwa muda kidogo tu. Ninyi mlio kwenye viti vyenu ketini kimya kabisa, kwa muda kidogo tu, tunawafuatilia, pia. Hiyo ni kweli. Tunakuja katika Jina la Yesu. Ninyi mnaosimama nje, tunawafuatilia, tukija katika Jina la Bwana Yesu. Ninachoshwa na maungamo haya mabaya na ya nusu-nusu, hebu tuwe makini na Mungu. Mungu aliliahidi. Mungu asipotimiza Neno Lake, Yeye si Mungu; Yeye hulitimiza Neno Lake kwa hiyo Yeye ni Mungu.

²⁰³ Wakati mmoja walipokuwa wamesimama, Daudi alikuwa akizungumza, Israeli walikuwa wakitetemeka, adui alikuwa langoni, sikilizeni jinsi lilivyo la Kimaandiko, na Daudi alipokuwa angali akinena, bila kujua yaliyokuwa yakitukia, Roho alishuka juu ya mtu fulani naye akatabiri, na kasema, “Shuka uende ukalale mahali fulani, ukavizie.” Nao, adui alijishambulia mwenyewe hata akafa papo hapo. Hilo lilisababisha mchafuko, nao wakajipiga wenyewe, nao wakaingia tu, wakateka nyara.

²⁰⁴ Sikilizeni, ninyi mlioketi huko nje kwenye kusanyiko, si lazima uwe hapa juu, kuwa tu na imani na umwamini Mungu. Mnajua kitakachotukia? Mungu atamfanya adui akuache papo hapo ulipo, mchafuko utaingia, hatajua mahali alipo.

²⁰⁵ Mtu anazungumza, na kusema, “Lisikieni Neno la Bwana, kinywa cha Bwana kimenena usiku wa leo,” na kadhalika namna hiyo, na kuwaambia la kufanya, kutii amri za Bwana. “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: Katika Jina Langu watatoa pepo, watanena kwa lugha mpya; wataweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya.” Mambo haya yote yameahidiwa, ni kazi ya Mungu, na Yeye ndiye Mfalme. Amina.

²⁰⁶ Hivi hamupendi, kumsifu? Ni wangapi wanaompenda? Wakati wakikusanyika, hebu na tuketi kimya kabisa vitini mwetu sasa, wakati wakiandaa mstari wa maombi. Hebu tuimbe wimbo huu, vema, *Nampenda*. Vema.

Nampenda, . . . (. . . ? . . .)
 . . . Yeye alinipenda kwanza
 Na kununua wokovu wangu

Mtini Kalvari.

²⁰⁷ Ninataka kuwaomba ninyi nyote katika mstari wa maambi neno moja, ninyi nyote mlio kwenye mstari wa maambi, wagonjwa, wahitaji: Umeomba hili, kwa uaminifu? Umeuomba ugonjwa wako? Ikiwa mmefanya hivyo, inueni mikono yenu, umeuomba. Unaamini uliuomba kwa bidii, ni mapenzi ya Mungu kukuponya? Kama umefanya hivyo, inua mkono wako. Kama uliomba kwa bidii juu yake, itatendeka. Hakuna ila jambo moja la kufanya basi, ni kuutupilia mbali kutoka kwako unapopitia hapa. Loo, jamani!

²⁰⁸ Ninahofia kusanyiko litafikiri kwamba mwinjilisti pekee ndiye aliye na mamlaka ya kufanya hivi, ninataka kundi la wahubiri, waje hapa pamoja nami, ninyi wahudumu wa ukombozi mnaoamini jambo hili, njoni hapa, msimame pamoja nami kwa dakika moja. Njoni hapa, ndugu. Simameni tu, fanyeni mstari mdogo hapa. Njoni, ndugu, yeyote wenu, njoni hapa, na msimame hapa; mpate kuona ya kwamba ni wahubiri, pia. Mimi si... Si mimi tu, ndugu zangu hapa, wao—wao wana... wao wamekusudiwa kufanya hivi kadiri nilivyokusudiwa, ama mtu mwingine yeyote, wao ni watumishi wa Mungu. Hilo ni zuri.

²⁰⁹ Sasa, sasa nitawaambia tufanye nini, watu wanasema, ndugu, kwamba wote wameomba hili, wote wako tayari, basi kama waliuomba, wakauomba kabisa, kuna jambo moja tu lililosalia, hilo ni kumtoa adui anapopitia hapa. Si lazima uwaombee, tayari wameomba. Hiyo ni kweli? Mnaona? Ili kwamba mwone si udanganyifu, si huo, ni nguvu za Mungu katika Neno Lake. Watu hawa ni watu waliotiwa mafuta, ni watu wa Mungu, nao wanaomba, pia. Sasa, niwaambie nini, kama wameuomba, hakuna haja ya sisi kuomba, wawekeeni tu mikono na kumwondolea mbali adui kutoka kwao.

²¹⁰ Tazameni, enyi kondoo wadogo, tunawafuatilia. Mko tayari kurudi? Hebu turudi kwenye afya njema usiku wa leo. Kila mtu awe na kicho kabisa.

²¹¹ Vipi kuhusu kufanya mistari miwili papa hapa? Na hebu tupitishie hawa, kila mtu apite, na kuomba... na kumtoa tu adui. Useme tu, “Shetani, tutaninii...” Unasemaje? [Ndugu fulani anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Vema, tutafanya mstari mmoja basi. Vema, ninyi ndugu sogeeni papo hapo, ninataka kila mmoja wenu wanaume awawekee watu hawa mikono wanapopita karibu nami.

²¹² Ninataka kila mtu huko nje aombe wakati mstari huu unapopita, nami ninaamini mtaona utukufu wa Mungu. Je, mtainama pamoja nami na kuomba pamoja nami? Kila mmoja wenu akina Daudi sasa mkiwa na kombeo lenu, njoni huku. Sasa, siamini katika kulenga risasi kombo. Kama hujalenga shabaha ya—yako vizuri, ilenge vilivo sasa hivi. Hebu—hebu twende tuka—tukamalizie.

²¹³ Angalieni hapa, maskini kondoo wa Mungu, si mapenzi ya Mungu kwamba yeyote kati yao awe mgonjwa, nao wameomba kwa bidii, kitu pekee wanachohitaji ni usaidizi kidogo, huo tu ndio wanaohitaji. “Jina Langu watatoa pepo.” Amina. Mnaamini hilo semeni, “Amina.”

²¹⁴ Shetani, afadhali uwaachilie, wanaenda zao.

²¹⁵ Hebu sote na tuinamishe vichwa vyetu sasa, na hebu kusanyiko hili, watu hawa watembee moja kwa moja kupitia hapa. Na mnapopitia hapa, kila mmoja wenu, wakati mhudumu wa kwanza atakapokugusa, inua mkono wako, umsifu Mungu imekwisha. Njoo moja kwa moja kupitia hapa, nawe utashuka kutoka kwenye jukwaa hili ukiwa mtu mwenye furaha sana uliyewahi kuwa. Tumekuja kukuchukua. Uko tayari kwenda? Vema. Na tuombe sote sasa huku vichwa vyetu vimeinamishwa.

²¹⁶ Njoo moja kwa moja huku, Mchungaji Weston, panda huko juu sasa, waguse watu wanapopita.

²¹⁷ [Ndugu Branham anawaombea wale walio kwenye mstari wa maombi, mengi ya maneno yake hayatambuliki—Mh.]

Katika Jina la Bwana Yesu, ibilisi huyu na atoke. Amina.

Katika Jina la Bwana Yesu, ibilisi huyu na atoke.

...?...Toka, Shetani...?...

Katika Jina la Yesu ibilisi na atoke.

Katika Jina la Yesu ibilisi na atoke.

Katika Jina la Yesu jalia...?...

²¹⁸ Iweni katika maombi kila mtu, sasa ombeni, ombeni, huyu ni mtu fulani, huyu ni kondoo anayepita sasa. Ombeni na mketi tu kimya, tulieni kimya kabisa na kuomba.

Katika Jina la Yesu na aponywe...?...

Tujalie, Bwana...?...

Bwana, ninamfuatilia. Katika Jina la Yesu, ibilisi na amwachilie...?...

Tunakufuata, Shetani. Mwachilie!...?...

²¹⁹ Mnampenda? Sasa iweni na kicho kabisa, ketini tu kwa dakika moja. Ninaamini kwa uchaji kwa moyo wangu wote na yote yaliyo ndani yangu ya kwamba Yesu Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai, anamponya kila mmoja wao. Mnaamini pamoja nami? Ninaamini maombi ya imani ambayo yameombwa juu yao. Sababu ya mimi kufanya hivyo, ili kwamba kusanyiko hili na makusanyiko yenu hapa, watu hawa wa Mungu wanaosimama hapa, wahudumu waliotiwa mafuta na Roho Mtakatifu, wana haki vivyo hivyo, mamlaka ya kuwaombea wagonjwa na kutoa pepo, kama mtu mwingine yeyote alivyo nayo ulimwenguni. Sasa, mnaamini jambo hilo? Vema.

220 Sasa, ni wangapi walio humu ndani ambao ni wagonjwa na hawana kadi ya maombi, nawe unataka Mungu akuponye? Inua mkono wako. Bado ni kundi kubwa. Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana. Mnaamini hilo?

221 Hizi ni leso, ninaziombea, muda kidogo tu. Ninamngojea Roho Mtakatifu afanye jambo fulani. Nilifikiri labda angenionyesha mtu fulani huko nje kwenye kusanyiko, ambaye mngemwona, kila mmoja anayepita, kwamba watu hawa, huenda wasiweze kuona—kuona maono, hawakuzaliwa kwa kusudi hilo, bali wana Roho Mtakatifu yeye yule, Mungu yeye yule. Mnaona?

222 Lakini sina elimu yoyote, baadhi ya watu hao ni werevu, lakini msifikiri wao ni wana wa Kishi hata hivyo, wao ni watu wanaoamini katika uponyaji wa Kiungu, wanaomwamini Mungu wa Mbinguni, wao ni watu hodari, bila shaka ndivyo walivyo. Nao—nao wanaamini jambo hili, wasingessimama hapa kuwaonyesha wanaliamini. Ninataka kusanyiko lao, kabla kusanyiko hili halijafumukana, na baadhi yenu mwe mnaenda nyumbani, ninawatakeni mjue ya kwamba mchungaji wenu ana mamlaka yale yale.

223 Sasa, ninataka kuwaonyesha ya kwamba hii ni kweli, ya kwamba Mungu alifanya ahadi, Yeye angali ni Mungu. Sasa ninyi ombeni na kuamini. Ninyi huko nje kwenye kusanyiko, angalieni kama Roho Mtakatifu anatia mafuta, angalieni kama Yeye angali hapa. Amina. Loo, napenda hili! Loo, Yeye si ni wa ajabu? Ninajua tu Yeye yu pamoja nasi. Omba tu, na kusema, “Bwana, nisaide, saidia kutokuamini kwangu.”

224 Ninamwona maskini mwanamke mmoja ameketi papa hapa chini ametiwa uvuli wa mauti. Hawezi kuishi Mungu asipomsaidia. Unajua hilo, sivyo, dada? Wewe, kansa, maskini ukingo mweupe wa maua unaozunguka kofia yako. Je, una kadi ya maombi, mama? Huna. Hujapata kabisa. Vema, bwana, huhitaji yoyote. Hiyo ni kweli, huo ndio unaokusumbua, kuna kivuli cheusi kinachoning’inia juu—juu yako. Je, unaiamini mimi kuwa ni nabii wa Mungu?

225 Basi, Shetani, katika Jina la Yesu Kristo, mwachilie! Ninakuja kukutana nawe.

226 Huyu hapo anaenda. Kile kivuli kilimwondokea, jambo fulani lilimfanyikia. Sasa, Roho Mtakatifu yeye yule anaweza kumwambia mambo hayo, hivi hujui Yeye amemponya?

227 Unajisikia umeponywa, dada? Simama kwa miguu yako. Amina.

228 Haya basi. Haya basi. Kama tu utakuwa na imani na kuamini, “Mambo yote yanawezekana kwao waaminio. Kama unaweza kuamini!” Hiyo ni kweli?

229 Ninamwona maskini mama mmoja ameketi papa hapa nyuma akiniangalia. Sijawahi kumwona maishani mwangu, lakini kuna . . . Hivi hamwezi kuona ile Nuru ikining'inia juu ya mwanamke huyo? Papa hapa. Anaomba, anaugua, ana shinikizo kuu la damu, ana vivimbe. Yeye hatoki hapa, ametoka Chicago. Unataka kwenda ukapate afya sasa, dada? Vema. Simama kwa miguu yako, maskini uliye na nywele nyekundu hapo. Nenda nyumbani, uwe mzima, Yesu Kristo alikuponya.

230 Unayo, pia, dada, kwenye shida yako, pia. Mungu akubariki. Nenda nyumbani sasa, uwe mzima, Yesu Kristo akuponye.

231 Unaamini kwa moyo wako wote? Mtu fulani aombe, mtu fulani aseme tu, "Bwana, jalia niguse vazi Lako." Siwajui watu hawa.

232 Naam, wewe, wewe si mgonjwa, bali unamwombea rafiki yako, mtu huyo. Una kadi ya maombi? La, huna yoyote. Unaniamini mimi kuwa ni nabii wa Mungu? Unaamini? Nisingejua hilo, hiyo ni kweli? Unaamini ugonjwa huo wa kupooza utamwacha rafiki yako? Unaamini jamaa huyo atapona? Unaamini? Inua mkono wako basi, utikise kwa Mungu. Vema. Naomba upokee tu kile ulichoomba.

233 Vipi kuhusu mtu fulani upande huu? Unaamini kwa moyo wako wote? Mtu fulani hapo anayeteseka, usiye na kadi ya maombi inua mkono wako. Sema tu, "Ninaamini."

234 Vipi kuhusu hilo, bwana, unaamini? Unaniamini mimi kuwa ni nabii wa Mungu? Una ngiri, mpasuko. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Wewe pia hutoki hapa, sivyo? Toledo. Hiyo ni kweli. Sikujui. Hiyo ni kweli? Inua mkono wako kama hiyo ni—hiyo ni kweli, yote hayo ni kweli. Vema. Kama unaamini, nenda nyumbani ukapone.

235 Ninakupa changamoto katika Jina la Yesu kuamini Mfalme yupo hapa!

236 Maskini mama huyu aliyeketi hapa nje mwishoni, akiomba, hajiombe mwenyewe, anamwombea mama yake aliyeketi nyuma kutoka hapa pale. Hiyo ni kweli. Vidonda vinavyotokwa na damu, amekuwa hospitalini. Vema. Amini sasa na Mungu atakuponya. Amina.

Unaamini kwa moyo wako wote? Pokea. Amina.

Dada, nenda nyumbani sasa na uwe mzima.

237 Mnaona, hilo ndilo linalohitajika, mtu kuomba.

238 Hiyo ilikuwa ni nini basi, Yeye alisema huo ulikuwa kitu gani, vidonda? Huyu ni pepo wa kansa aliyepita. Sasa hebu kidogo. Mtu fulani anaomba.

239 Loo, amelala huko nyuma kwenye machela. Alikusikia, alikusikia . . . ? . . . Huyu pepo wa kansa alipitia hapa wakati huo. Kama unaamini kwa moyo wako wote, unaniamini kama

mtumishi wa Mungu, ninakwambia, katika Jina la Yesu Kristo, simama kutoka kwenye machela hiyo, nenda nyumbani. Amina.

²⁴⁰ Yeye anafanya hivyo! Unaamini kwa moyo wako wote? Ni wangapi zaidi wanaoamini? Simameni kwa miguu yenu, simameni kwa miguu yenu. Huyu hapo, mzima kabisa. Unaamini kwa moyo wako wote? Simameni kwa miguu yenu na kumpokea Bwana Yesu, kila mmoja wenu. 

60-0610 Mfalme Aliyekataliwa
Miami Valley Chautauqua Campgrounds
Chautauqua, Ohio Marekani

SWAHILI

©2026 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org